# Nipashe

Jumatatu Desemba 21, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580436

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710





UKURASA 11

**CHADEMA** yawasubiria kina Mdee Desemba 27

UKURASA 3



**TEC** yamlilia Askofu Anthony Banzi

UKURASA 2

# Maeneo haya hatari kwa uporaji simu, mikoba Dar



**VIBAKA** watumia bodaboda...*Endelea Uk. 4*



Baadhi ya abiria wanaokwenda mikoa mbalimbali wakisubiri usafiri, kutokana na uhaba wa mabasi katika stendi ya mabasi Ubungo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

UKURASA WA 5

## WAATHIRIKA WA TETEMEKO KAGERA WAPIGWA JEKI

SHIRIKA la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), na serikali ya Afrika Kusini, wametoa msaada wa ujenzi wa vyumba vya madarasa pamoja na majengo katika hospitali mbalimbali mkoani Kagera wenye thamani ya Sh. bilioni 2.1...

UKURASA WA 5

## KAMPUNI ZA UTURUKI ZAONYESHA NIA KUWEKEZA

KAMPUNI tano kutoka Uturuki zimeonyesha nia ya kuwekeza nchini kwenye sekta ya kilimo, ujenzi wa viwanda vya kutengeneza pampas za watoto na watu wazima, vifaa tiba, dawa na vifaa vya kilimo....

# Serikali yakataza kupiga risasi wananchi hifadhini

UKURASA 2

## Mavazi ya wahitimu yamkera Katibu Mkuu

UKURASA 2

**MICHEZO** KAPOMBE AAHIDI KUFA KUPONA KWA PLATINUM UK. 23

MAONI, KATUNI UK. 6

# Wanaopiga risasi wananchi hifadhini waonywa

**Na Richard Makore,** MWANZA

SERIKALI imepiga marufuku na kuwaonya watumishi wa Idara ya Wanyamapori wanaopiga risasi watu wanaowakamata wakifanya shughuli mbalimbali ikiwamo ujangili katika hifadhi za taifa, kuacha badala yake watumie sheria kukabiliana nao.

Kadhalika, watumishi wa idara mbalimbali zilizo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, wametakiwa kubadilika na kuachana na vitendo vya rushwa.

Agizo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki iliyopita na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, alipokutana na watumishi wa idara mbalimbali zilizo chini ya wizara hiyo katika Chuo cha Wanyamapori cha Pasiansi, jijini Mwanza.

Akizungumza na watumishi hao, Masanja alisema kuna malalamiko mengi katika baadhi ya hifadhi kwa maaskari kuwapiga risasi na kuwaua watu wanaowakuta ndani ya hifadhi na kuonya kuanzia sasa waache. “Nimepata malalamiko mengi ya askari wetu wa wanyamapori kuwapiga risasi na kuwafanyia vitendo vibaya watu wanaowakuta ndani ya hifadhi, sasa vitendo hivi mviache,” alisema.

Alisema serikali inatambua kazi kubwa inayofanywa na askari hao katika kulinda rasilimali za taifa, lakini ulinzi huo usiende kinyume cha haki za binadamu.

Masanja alisema askari hao watumie mbinu zao za kijeshi kuwakamata watu wanaowakuta ndani ya hifadhi na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria.

“Najua majangili nao wamejipanga na ukikaa vibaya watakumaliza huko porini, lakini hiyo isiwe sababu ya kuwapiga risasi badala yake mtumie sheria zaidi,” alisema.

Kuhusu kutangaza vivutio vya utalii katika Mkoa wa Mwanza, Masanja alisema bado havijatangazwa vya kutosha kwa wadau mbalimbali ikiwamo wananchi wa kawaida.

Aliwataka watumishi hao kutumia ujuzi wao kutangaza vivutio vilivyopo jijini humo ili kuongeza mapato ya serikali na kupanua sekta hiyo kama Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020/2025 inavyoelekeza.

Kuhusu watumishi hao kujihusisha na vitendo vya rushwa, Masanja alikemea tabia hiyo na kuwaonya kujiepusha navyo.

Alitoa mfano kwa baadhi ya watumishi wanaokamata mkaa badala ya kuwapiga faini wahusika, wanaamua kakaa nao mezani na kupanga ‘dili’ na kisha kuwalipisha kiasi kidogo ambacho pia wanakipunguza na kukiweka mifukoni mwao na kisha kupeleka ‘kiduchu’ serikalini.

Alisema tabia hiyo inachangia kurudisha nyuma maendeleo ya Watanzania na kwamba serikali hii hakuna mtu atakayepona kama anakwenda kinyume cha taratibu.

Akizungumzia umuhimu wa watu kunufaika na rasilimali zao, Masanja alitaka kuharakishwa ufunguaji wa bucha za nyamapori katika maeneo mbalimbali ya nchi ili wananchi waweze kuipata.

Alisema hatua hiyo itasaidia kupunguza ujangili katika maeneo mbalimbali ya hifadhi nchini na lengo ni kuhakikisha wanafaidika na rasilimali zao.

Baadhi ya watumishi walio chini ya wizara yake aliokutana nao ni kutoka Chuo cha Wanyamapori cha Pasiansi, Wakala wa Huduma za Misitu Nchini (TFS), TANAPA, TAWA pamoja na askari wa wanyamapori.



Mtendaji wa Kata ya Kolandoto, Manispaa ya Shinyanga, Mwakaluba Wilson, akiongoza wananchi wa kata hiyo, kuchimba msingi kwa ajili ya ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa katika Shule ya Sekondari ya Kolandoto, ili kupunguza upungufu wa vyumba hivyo, uliopo shuleni hapo. **PICHA: MARCO MADUHU**

# TEC yamlilia Askofu Banzi

**Na Elizabeth Zaya**

ASKOFU wa Jimbo Katoliki la Tanga, Antony Banzi, amefariki dunia jana katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), alikokuwa akipatiwa matibabu.

Taarifa iliyotolewa jana na Katibu wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Padri Charles Kitima, ilieleza kuwa Askofu Banzi alifariki dunia asubuhi na kwamba taratibu za mazishi zitatangazwa baadaye.

“Baraza linatoa pole kwa familia yote ya Mungu jimboni Tanga na Kanisa Katoliki Tanzania kwa ujumla kwa msiba huu mkubwa, Baraza linamwombea kwa Mungu ili roho yake ipumzike kwa amani mbinguni pamoja na watakatifu.”

Kufuatia msiba huo, Chama cha ACT-Wazalendo kupitia Naibu Katibu wa Habari, Uenezi na Mahusiano kwa Umma, Janeth Rithe, kimesema kimeshtushwa na kuhuzunishwa na taarifa za kifo cha Askofu Banzi na kwamba kitamkumbuka kwa utumishi wake na upendo kwa taifa.

“Katika uhai wake, Askofu Banzi amelitumikia taifa kiroho kwa upendo mkubwa, Chama cha ACT-Wazalendo kinatuma salamu za pole kwa Kanisa Katoliki Jimbo la Tanga, kwa Wakatoliki wote nchini na kwa watu wote walioguswa na kwa namna moja ama nyingine.”

# Mavazi ya wahitimu yamkera Katibu Mkuu

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

WANAVYUO wametakiwa kuvaa mavazi yenye staha na yanayozingatia maadili ili kuwa kioo kizuri kwa jamii inayowazunguka.

Wito huo ulitolewa na Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mary Makondo, kwenye mahafali ya 38 ya Chuo cha Ardhi Tabora, baada ya kuwaona baadhi ya wahitimu wa kike wakiwa wamevaa nguo zisizo na staha.

Alisema hata katika utumishi wa umma kuna kanuni za mavazi ambazo mtumishi anatakiwa kuzifuata, na kwa wanachuo ni vema wakavaa nguo ambazo zina staha kwa kuwa nao ni watumishi watarajiwa.

“Mimi kama mzazi niseme tu tuangalie tulivyo, walimu wametufundisha tumepata elimu muda tuliokaa tubadilike... the way you dress (namna mlivyovaa) inakuonyesha ulivyo,” alisema na kuongeza: “Hata tukisema mtoe majoho sasa hivi, ni aibu tupu, wengi mtaabika, lazima mbadilike mvae vizuri.”

Alisema baadhi ya wahitimu nguo walizovaa zinaweza kuwasababishia kukosa ajira kwa kuwa ni kielelezo cha walivyo na hata wakipewa kazi ndivyo watakavyokuwa.

“Hata hivi sasa tukisema tuwatenge kwa ajili ya usahili wa kutafuta wahitimu wa kuwapa ajira, kuna baadhi yenu tutawaachia kwa jinsi walivyovaa... lazima uangalie ulivyokuja kutoka kwenu ulikuja vipi na leo unaondoka na tabia gani. Tubalike, tunatakiwa kuonekana kwa kumwonekano mzuri,” aliongeza.

Katika hatua nyingine, aliwataka wahitimu watakaopata fursa ya ajira kuwa waadilifu na wazalendo na kuepuka tamaa ya kupata utajiri wa haraka, ambao utawasababishia kuishia kifungoni.

“Ule mtazamo wa kusema nataka kutajirika haraka mafaili yapotee utafungwa...epukeni vitendo vya wizi, dhuluma, ubadhirifu, kuomba na kupokea rushwa, fanyeni kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozi ya taaluma zenu,” alisema.

Naye Mkuu wa Chuo cha Ardhi Tabora, Biseko Musiba, alisema kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya wataalamu wa sekta ya ardhi hasa katika ngazi ya mafundi sanifu, wameongeza idadi ya wanachuo.

# CHADEMA yawasubiria kina Mdee Des. 27

**Na Elizabeth Zaya**

ZIKIWA zimebaki siku sita, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimesema kinasubiri Desemba 27 kifunge mlango ambao kimetoa kwa wabunge wa viti maalum 19, akiwamo aliyekuwa Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake (BAWACHA), Halima Mdee (pichani), kukata rufani ya kupinga kuvuliwa uanachama wa chama hicho.

Mdee na wenzake 18 waliovuliwa uanachama wa chama hicho baada ya kuapishwa kuwa wabunge wa viti maalum kupitia chama hicho kinyume cha makubaliano na chama chao, walisema wanapanga kukata rufani hiyo kwa Baraza Kuu la CHADEMA kupinga uamuzi huo.

Akizungumza na Nipashe jana, baada ya kuulizwa kama wamepata barua kutoka kwa kina Mdee ya kukata rufani hiyo, Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa Chama hicho, John Mrema, alisema wao wanachosubiri ni Desemba 27 kufunga mlango huo kwa mujibu wa Katiba ya chama chao.

"Waulizeni wao wenyewe, maana isiwe kama tunawalazimisha, sisi tunachosubiri ni Desemba 27 tufunge mlango," alisema Mrema.

Kwa mujibu wa CHADEMA, kina Mdee wanatakiwa kukata rufani hiyo ndani ya siku 30 kuanzia siku ya kuvuliwa uanachama endapo watakuwa na nia ya kufanya hivyo.

Wakizungumza na waandishi wa habari Desemba mosi mwaka huu, Mdee na wenzake walisema watakata rufani kwa Baraza Kuu la chama hicho kupinga uamuzi huo.

Hata hivyo, mpaka Desemba 14, mwaka huu, baada ya kuzungumza na Nipashe walikuwa bado hawajakata rufani hiyo, huku wakisema bado wana muda wa kutosha wa kufanya hivyo.

"Bado muda upo tutakata tu rufani kama tulivyosema pale kwenye mkutano na waandishi wa habari," alisema hivyo aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa Baraza hilo, Hawa Mwaifunga, wakati akizungumza na gazeti hili Desemba 14.

Kwa ujumla wao, wakiwa katika mkutano na waandishi wa habari Desemba mosi, kina Mdee walidai kupokea rasmi barua ya



kuvuliwa uanachama huo Novemba 30, mwaka huu.

Pia walisema wataendelea kuwa wanachama wa hiari wa chama hicho kutokana na mapenzi waliyonayo kwa chama chao.

CHADEMA ilitangaza kuwavua uanachama wanachama wake 19 Novemba 27, baada ya kwenda bungeni kuapishwa kuwa wabunge wa viti maalum, wakati chenyewe kikidai kutoutambua uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu na kutovitambua viti hivyo maalum vya ubunge walivyopata katika uchaguzi huo.

# Madhehebu ya dini yahimizwa uwekezaji

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka viongozi wa dini nchini kuangalia fursa zilizopo nje ya nyumba za ibada, ili wawekeze katika miradi mbalimbali itakayo wezesha Taifa kuendelea kukuza uchumi wake.

Aliyasema hayo, jana, jijini Dodoma wakati akitoa hotuba yake katika ibada ya kumsimika Askofu Mkuu wa Kanisa la Philadelphia Gospel Assembly, Dk. Yohana Masinga.

Alisema kutokana na serikali kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya uwekezaji, viongozi wa dini hawana budi kuangalia fursa zilizopo ili wawekeze katika miradi mbalimbali.

Alisema pamoja na taasisi za dini kuwekeza katika sekta ya elimu pamoja na afya, bado zipo fursa nyingi ambazo kama zitatumika zinaweza kusaidia kuinua uchumi wa makanisa na taifa kwa ujumla.

"Serikali hivi sasa imeweka mazingira mazuri sana kwa ajili ya uwekezaji, hivyo basi niwaombe viongozi wa dini kuangalia fursa zilizopo kama vile kwenye sekta uchimbaji wa madini chuma ambayo hivi sasa yanahitajika sana duniani au katika sekta ya viwanda," alieleza Majaliwa.

Aidha, aliziagiza mamlaka zinazohusika na upangaji wa miji kuhakikisha kila zinapo andaa michoro ya mipango miji kutenga maeneo kwa ajili ya nyumba za ibada.

"Lazima maeneo rasmi kwa ajili ya nyumba za ibada yatengwe kila michoro ya mipango miji inapoandaliwa, kutotenga maeneo ya ibada ni kunyima watu haki yao ya kuabudu na maeneo hayo ni lazima yapewe madhehebu ya dini na siyo vinginevyo," alisema Majaliwa.

Askofu wa kanisa hilo, Kanda ya Ziwa, Stephen Mhaya, akisoma risala ya kanisa hilo, alisema kuwa kanisa hilo limetimiza miaka 30, toka kuanzishwa kwake.

Askofu Mhaya, alisema kuwa kanisa hilo lina matawi zaidi ya 150 nchini, matano Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burindi manne, Asia manne na Marekani 2.

Alisema, kusimikwa kwa Askofu huyo mkuu ndiye atakayekuwa mkuu wa makanisa yote kwa mujibu wa katiba yao.

Vile vile, katika ibada hiyo kanisa hilo limempatia Rais John Magufuli, tuzo ya utumishi uliotukuka kutokana na miradi mikubwa ambayo ameitekeleza katika utawala wake.

# PURA: 30% tu ya mafuta na gesi ndiyo imetafutwa

**Na Elizabeth Zaya**

> **"Na tumeona kwamba kuimarika kwa mifumo ya kisheria na udhibiti katika uendeshaji wa sekta ndogo hii, kumechangia kuongezeka kwa ushiriki wa wazawa katika shughuli hizi," alisema Sangweni.**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), imesema mpaka sasa utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika maeneo yote yaliyofanyiwa utafiti na kugundulika kuwa na rasilimali hiyo nchini ni asilimia 30 tu.

Akizungumza katika semina ya waandishi wa habari iliyofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa PURA, Charles Sangweni, alisema asilimia 70 ya mafuta na gesi hiyo bado haijatafutwa.

"Utafiti wa awali ni kwamba kati ya kilomita 534,000 ndizo zenye mafuta na kilomita 160,000 au asilimia 30 ndizo zimetafutwa mpaka sasa, kwa hiyo ambazo hazijatafutwa katika zile zilizogundulika bado ni asilimia 70," alisema Sangweni.

Alisema mpango ni kuhakikisha kwamba ifikapo mwaka 2022 wawe wamefika katika hatua kubwa zaidi ya utafutaji wa mafuta na gesi hiyo katika maeneo yote yaliyogundulika.

Alisema mipango ya kutafuta mafuta na gesi hiyo iko vizuri, na kwamba watahakikisha kwamba yote inatafutwa kwa ajili ya manufaa ya nchi na wananchi wote.

Alisema mamlaka hiyo imekuwa ikisimamia kuhakikisha rasilimali ya mafuta na gesi asilia nchini inazalishwa kwa tija na kwa manufaa ya wote.

"Na tumeona kwamba kuimarika kwa mifumo ya kisheria na udhibiti katika uendeshaji wa sekta ndogo hii, kumechangia kuongezeka kwa ushiriki wa wazawa katika shughuli hizi," alisema Sangweni.

Alisema kwa sasa idadi ya wataalamu wazawa wanaofanya kazi katika sekta hiyo imezidi kuongezeka tofauti na ilivyokuwa katika miaka ya nyuma.

Alisema katika kuboresha zaidi sekta hiyo, tayari wameshapeleka maombi ya kufanyia maboresho ya sheria katika sekta hiyo, ili kutoa fursa kwa watu mbalimbali kuwekeza katika shughuli hizo wakiwamo wa kutoka ndani na nje ya Tanzania.

"Lengo ni kuwa mdhibiti wa kimataifa wa mkondo wa juu wa petroli anayesimamia shughuli na rasilimali hizi kwa manufaa ya kizazi cha sasa na cha baadaye, kudhibiti shughuli za mkondo wa juu wa petroli kwa uwazi, weledi na ufanisi ili kuchangia katika ustawi wa jamii na kiuchumi kwa Watanzania," alisema Sangweni.

NHC
SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA
TUNAJENGA TAIFA LETU

## TAARIFA KWA WAPANGAJI WA NYUMBA ZA NHC WANAODAIWA KODI NA MALIMBIKIZO

1. Shirika la Nyumba la Taifa linawashukuru wapangaji wake walioweza kulipa kodi na malimbikizo yao baada ya kupewa notisi ya siku kumi na nne (14) ya kulipa kodi na malimbikizo wanayodaiwa. Aidha, wapo wapangaji wachache ambao bado wanadaiwa kodi na malimbikizo hadi sasa.
2. Kwa mara nyingine, Shirika linatoa siku thelathini(30) kwa wapangaji wanaodaiwa kodi na malimbikizo kufika katika ofisi za Shirika zilizo karibu nao ili kulipa kodi na malimbikizo wanayodaiwa.
3. Shirika linawashauri wapangaji wote kutumia fursa hii kulipa madeni yao na baada ya muda huu uliowekwa kukamilika, Shirika litatumia taratibu za kisheria kukusanya kodi na malimbikizo yanayodaiwa wapangaji ikiwemo kukamata na kupiga mnada mali za wapangaji ili kufidia kodi na malimbikizo yanayodaiwa. Aidha, baada ya muda huu kupita, Shirika halitasita kutangaza kwenye vyombo vya habari majina ya wadaiwa wote sugu ili umma ufahamu watu wanaokwamisha maendeleo ya Shirika na Taifa kwa kutokulipa kodi.
4. Tunashukuru wapangaji wote wanaotimiza wajibu wao wa kulipa kodi kwa wakati na kuliwezesha Shirika na Taifa kuwaletea maendeleo watanzania kwenye sekta ya nyumba.

**IMETOLEWA NA: OFISI YA MAWASILIANO NA HUDUMA KWA JAMII**
**NHC-MAKAO MAKUU**

**SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA**
MAKAO MAKUU S.L.P 2977 | DAR ES SALAAM TANZANIA | SIMU: +255 22 2105001-5 | NUKUSHI: +255 22 2105000
BARUA PEPE: dg@nhctz.com | TOVUTI: www.nhctz.com
BARUA ZOTE ZITUMWE KWA MKURUGENZI MKUU

RIPOTI MAALUM

# Maeneo haya hatari kwa uporaji simu, mikoba Dar

## ■Vibaka watumia bodaboda...

Na Gwamaka Alipipi

MTANDAO wa wikipedia unaripoti kwamba Dar es Salaam mwaka huu inakadiriwa kuwa na wakazi milioni 6.702. Kuwapo kwa miundombinu ya uhakika wa usafiri na nishati sambamba na ofisi nyingi za serikali, kumewavutia wengi kuishi ndani ya jiji hilo la kibiashara.

Penye wengi pana mengi! Wingi wa watu ndani ya jiji hilo, umechangia kuwapo kwa matukio ya kihalifu, ukiwamo uhalifu wa kutumia silaha.

Lakini, iko wazi kwamba tangu Jeshi la Polisi lilipopewa agizo la kuwanyang'anya silaha majambazi, matukio ya wizi wa kutumia silaha za moto jijini yamepungua kwa kiwango kikubwa kama siyo kumalizwa.

Hata hivyo, kuna shida mpya ya wahalifu wanaopora simu na mikoba kwenye maeneo mbalimbali jijini, uhalifu wenyewe ukifanyika mchana 'kweupe'.

Uchunguzi uliofanywa na Nipashe kwa miezi kadhaa jijini, ukihusisha mahojiano na baadhi ya waathirika wa aina hjyo ya uhalifu huo jijini, umebaini baadhi ya wahalifu hao wanatumia pikipiki, maarufu bodaboda, kukwapua simu, mikoba ya kike na mabegi madogo, wakiamini ndani kuna kompyuta mpakato au fedha.

Madhara ya aina hiyo ya uhalifu yanahusisha siyo tu wahusika kupoteza mali zao, bali pia kupata matatizo ya kiafya kutokana na kuumizwa wakati wa harakati za kuporwa.

Waporaji hao ambao hukimbia kwa kasi pindi wakifanikiwa kukwapua simu na vifaa vingine tajwa, wanadaiwa kuvitumia vituo vya daladala jijini kama sehemu ya mitego ya mawindo yao.

Inadaiwa kuwa mbali na kutumia pikipiki, baadhi ya waporaji hukwapua simu wakati kunapokuwa na foleni ya magari, ambayo ni moja ya kero kubwa za jiji hilo kubwa Afrika Mashariki.

Nipashe ilimtafuta Mkuu wa Upelelezi wa Jeshi la Polisi Dar es Salaam, Camilius Wambura, ili kufahamu namna wanavyodhibiti matukio hayo na akikiri kuwapo kwa matukio hayo ya uhalifu na wanapambana nayo.

Alisema Jeshi la Polisi linafanyakazi usiku na mchana na matukio hayo yanapotokea wanayakabili.

"Jeshi la Polisi kazi yake ni kulinda wananchi na mali zao, hivyo hayo matukio hayo yanatokea mara kwa mara lakini sisi tunapambana nayo na kuyazuia," alisema.



Aidha, Kamanda Wambura aliwataka wananchi kuwa makini wanapotembea barabarani kwa kuweka mali zao vizuri.

Alisema mwananchi akiwa makini kwa kuhifadhi mali yake vizuri, matukio ya uporaji yatapungua, na kuwataka wanaoporwa kutoa taarifa kituo cha polisi kilicho jirani.

**MAENEO HATARISHI**

Maeneo yaliyotajwa kuwa ni hatarishi kwa uporaji huo ni Ubungo, Tazara, Mlimani City, baadhi ya mitaa ya Masaki, Oysterbay, Posta, Tabata, Mwenge na Tegeta, kwamba waporaji hao hukwapua simu wakati mtumiaji akiongea kwenye daladala, anatembea ama ameishika.

Maeneo mengine ni kandokando ya Barabara ya Sam Nujoma, Tandale kwa Mtogole, Sayansi (Mikocheni), Morocco, Riverside na Mbezi Mwisho.

Nipashe ilipozungumza na baadhi ya waathirika wa matukio hayo, walisema waporaji hao hutumia utaalamu wa hali ya juu kutekeleza dhamira yao.

Walisema waporaji hao mara nyingi hutumia pikipiki aina ya Boxer ambazo zina mwendo kasi na kuwa vigumu kukamatwa wanapotekeleza vitendo hivyo.

Mmoja wa waliowahi kuporwa simu, David James, alisema siku ya mkasa alikuwa akitoka kazini maeneo ya Mikocheni majira ya saa 11 jioni, na alipofika eneo la Mwenge alitoa simu mfukoni ili ampigie rafiki yake.

Akisimulia mkasa huo, James alisema alipoanza kuongea zilipita takribani dakika tatu, ghafla simu yake ikawa imepokwa na dereva pikipiki aliyepita kwa mwendokasi.

"Sikutarajia kama angeweza kunipora kwa sababu nilikuwa kituoni nimesimama na kulikuwa na watu wengi tukisubiri usafiri, kitendo cha mimi kugeuka ndicho kilimpa mwanya (kibaka) kukwapua simu yangu," alisema na kuongeza:

"Baada ya kunipora, alikimbia kwa mwendokasi, niliishia kumwangalia tu kwa sababu sikuwa na uwezo wa kumfukuza," alisema James.

Alibainisha kuwa waporaji hao hujibanza maeneo ambayo siyo rahisi kuwaona na mara nyingi wanakuwa kama wanatumia dawa aisee...yaani wanapora kwenye mazingira ambayo huyadhanii kabisa."

Mwathirika mwingine wa matukio hayo aliyejitambulisha kwa jina moja la Mwombeki, alisema: "Hawa watu ni kama wanatumia dawa aisee...yaani wanapora kwenye mazingira ambayo huyadhanii kabisa."

Akisimulia namna alivyoibiwa simu yake ya gharama kubwa, Mwombeki alisema siku hiyo alikuwa ndani ya daladala majira ya jioni akitokea kazini.

Alisema alikuwa amekaa kiti cha dirishani na alifungua dirisha kidogo ili apate upepo, kwa sababu daladala aliyokuwamo, ilikuwa imejaza abiria wengi.

Anaeleza kuwa walipofika eneo la Ubungo mataa, kukiwa na foleni, alitoa simu yake mfukoni kwa lengo la kupigia simu jamaa yake.

"Ile nimeanza kuongea tu... hata dakika tano haijafika ghafla nikasikia kwapu... simu imeondoka, yaani yule kibaka alikuwa kwenye pikipiki, lakini aliweza kuikwapua simu niliyokuwa nayo kwenye daladala, inavyoonekana alivyofika dirishani alisimamisha pikipiki," alisema Mwombeki.

Udadisi wa Nipashe ulihamia kwenye vituo vya pikipiki jijini na kuzungumza na baadhi ya madereva bodaboda ambao walikiri kuwapo kwa baadhi ya wenzao ambao wameacha kazi ya kubeba abiria na kujiingiza katika vitendo vya uporaji.

Walisema kuwa uwapo wa matukio hayo umeitia doa kazi yao na kusababisha madereva pikipiki wote kuonekana ni wezi, jambo ambalo siyo kweli.

Walisema kuwa hali hiyo imewasababishia kuogopwa na abiria, hata wakati mwingine kukosa abiria kutokana na abiria kulazimika kutumia teksi.

Mmoja wa madereva hao anayefanya shughuli zake eneo la Kimara Stop Over, Hassan Mwarabu, alisema: "Yaani sasa hivi ukipita na pikipiki kituoni, kila mtu anaficha simu, wengine wanakumbatia mikoba yao, tunaonekana wote ni wezi."

Alisema kuendesha bodoboda ni kama kazi zingine zinazoingiza kipato, lakini imeingiliwa na baadhi ya vijana ambao wanaendesha vitendo vya uporaji.

**KAULI YA POLISI**

Mkuu wa Upelelezi wa Jeshi la Polisi Jiji la Dar es Salaam, Wambura, akizungumzia hatua zinazochukuliwa na jeshi hilo kudhibiti uhalifu huo, alisema:

"Jeshi la Polisi kazi yake ni kulinda wananchi na mali zao, hivyo hayo matukio yapo na yanatokea kwa mara, lakini sisi tunapambana nayo kwa kuyazuia.

"Jeshi la Polisi linafanya kazi usiku na mchana na linafanya kazi vizuri, hayo matukio yakitokea tunayakabili. Kuna upungufu ambao hatuwezi kuzuia, lakini tunafanya kazi vizuri katika kuwalinda wananchi."

Kamanda Wambura aliwataka wananchi kuwa makini pindi wanapotembea barabarani kwa kuweka simu zao vizuri.

Alisema mwananchi akiwa makini kwa kuhifadhi mali yake vizuri, matukio ya uporaji yatapungua, akiwataka wanaoporwa, kutoa taarifa katika kituo cha polisi kilicho jirani.

HABARI KITAIFA

# UNDP, Afrika Kusini zasaidia athari za tetemeko ardhi Kagera

**Na Restuta Damian, BUKOBA**

SHIRIKA la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na Serikali ya Afrika Kusini, wametoa msaada wa ujenzi wa vyumba vya madarasa pamoja na majengo katika hospitali mbalimbali mkoani Kagera wenye thamani ya Sh. bilioni 2.1.

Msaada huo ni baada ya kutokea kwa tetemeko la ardhi mwaka 2016, kwamba vyumba 43 vya madarasa pamoja na majengo ya hospitali vimekabidhiwa.

Akipokea msaada huo, Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti (pichani), alisema utasaidia wanafunzi wanaotarajiwa kujiunga na kidato cha kwanza mwakani, ingawa kuna upungufu wa vyumba vya madarasa 250.

Naye Mratibu wa Maafa Mkoa wa Kagera, Issa Mlimi, alitaja maeneo yaliyoathiriwa na tetemeko hilo kuwa ni pamoja na Halmashauri za Wilaya za Bukoba, Missenyi, Karagwe, Muleba, Kyerwa na Bukoba Manispaa.

Alisema katika upande wa elimu, UNDP limefanikisha ujenzi wa madarasa 43, vyoo 17 vyenye matundu 56, nyumba za walimu tatu, ofisi za walimu kwa halmashauri zote sita zilizoguswa na tetemeko hilo.

Kuhusu sekta ya afya, Brigedia Jenerali Gaguti alisema UNDP imejenga wodi, jengo la mama na mtoto, jengo la wagonjwa wa nje pamoja na nyumba ya watumishi.



Kwa upande wake mwakilishi wa Balozi wa Afrika Kusini nchini, Stella Dhlomo, alisema miundombinu iliyokamilika itunzwe vizuri ili iweze kudumu na kufikia malengo kwenye sekta ya elimu.

Aliongeza kuwa ujenzi huo umezingatia uimara na tahadhari ya maafa endapo yatatokea, kwamba ni jukumu la serikali kuyatunza.

# Kampuni za Uturuki zaonyesha nia kuwekeza

**Na Elizabeth Zaya**

KAMPUNI tano kutoka Uturuki zimeonyesha nia ya kuwekeza nchini kwenye sekta ya kilimo, ujenzi wa viwanda vya kutengeneza pampasi za watoto na watu wazima, vifaa tiba, dawa na vifaa vya kilimo.

Ujumbe huo ukiongozwa na Balozi wa Tanzania nchini Uturuki, Prof. Elizabeth Kiondo, ulifika nchini kuona fursa zilizopo nchini.

Mkurugenzi wa Uhamasishaji Uwekezaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), John Mnali, akiwakaribisha wawekezaji hao, alisema wanahitaji uwekezaji zaidi katika eneo la kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, uvuvi, madini, ufugaji, vifaa tiba, dawa na maeneo mengine ikiwamo utalii.

Mnali aliwahakikishia wawekezaji hao kwamba serikali ipo tayari kuwapatia ushirikiano.

Alisema tayari sekta binafsi nchini zimeonyesha utayari wa kushirikiana na kampuni hizo katika kufanikisha uwekezaji huo, kwamba maeneo wanayokusudia kuwekeza ni miongoni mwa vipaumbele vya serikali.

Merve Safa mmoja wa wageni hao akizungumza na waandishi wa habari, alisema wako tayari kuwekeza katika maeneo mbalimbali ikiwamo viwanda vya kutengeneza pampasi za watoto, vifaa tiba, kilimo, zana za kilimo, viwanda vya nguo na vile vya kuunganisha zana za kilimo.

Merve alisema ujumbe huo pia umefika ili kukutana na wadau mbalimbali wanaohusika katika kutoa vibali vya kufanikisha uanzishaji wa uwekezaji wao Tanzania, ili kupata mwongozo zaidi wa kuwekeza katika maeneo wanayokusudia.

Alisema wawekezaji kutoka Uturuki wapo nchini na wamewekeza kwenye sekta ya viwanda, elimu, ujenzi, kilimo na madini.


Nestlé Good food, Good life

## TANGAZO LA UWAKALA

Kampuni ya Nestle, office ya Tanzania, inatafuta mawakala wa kusambaza bidhaa zake kwenye kanda na mikoa ifuatayo

- Kanda ya Kaskazini (Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara)
- Kanda ya Kati (Morogoro, Dodoma na Singida)
- Nyanda za juu Kusini (Iringa, Mbeya, Songwe, Rukwa na Katavi)

Tanahitaji wakala mwenye maono marefu ya kibiashara na kiu ya kukua na mwenye uwezo wa kukuza bidhaa zetu kupitia usambazaji wa rejareja na ukuaji wa wateja.Kampuni inaahidi mapato mazuri kwa wafanyabiashara watakaoshinda zabuni.

**Vigezo vinavyotakiwa kwa mawakala ni kama vifuatavyo:**

1. Uelewa mkubwa wa eneo husika, njia za mauzo, wateja na uwezo wa kujua makadirio ya mauzo kwa mwezi,nusu mwaka hadi mwaka mzima.
2. Dhamana ya benki ya shilingi milioni 300 za kitanzania toka kwenye benki maarufu hapa nchini
3. Mtaji usiopungua shilingi milioni 500 za kitanzania
4. Ofisi iliyounganishwa mtandao wa intaneti.
5. Ghala lenye nafasi ya kutosha angalau mita mraba 2000(sq)
6. Wauzaji mahiri wa bidhaa angalau 2 kwa ajili ya uchukuaji oda za wateja, 2 kwa kutumia magari na mtunza kumbukumbu mmoja.
7. Awe na uwezo wa kuwa na magari yafuatayo: Canter 2 (tani3) za kuuza mkoa kwa mkoa na magari madogo (Suzuki carry) angalau moja kwa kila mkoa uliotajwa hapo juu.
8. Awe na kampuni iliyosajiliwa Tanzania yenye rekodi nzuri ya ulipaji kodi pamoja na nakala za miaka mitatu za barua za ulipaji kodi (Tax clearance certificates)
9. Kampuni inayojishughulisha na usambazaji au yenye uzoefu na biashara za usambazaji bidhaa itakuwa kwenye nafasi nzuri ya kufikiriwa.

Maombi yepelekwe kwenye anuani ifuatayo kabla ya **tarehe 15 Januari 2021** yakielezea eneo husika la uwakala.

**Meneja maendeleo ya biashara**
**Nestle Tanzania**
**S.L.P. 105665**
**Dar es Salaam**
**Tanzania.**



**TUMAINI UNIVERSITY MAKUMIRA**
**P. O. Box 55, USA-RIVER, ARUSHA**
**Tanzania, East Africa**

## JOB VACANCIES

Tumaini University Makumira (TUMA) invites qualified applicants from recognized institutions of higher learning to be considered for employment in the following teaching posts:

1. **Lecturers or Assistant Lecturers in Physics**
2. **Lecturers or Assistant Lecturers in Chemistry**
3. **Lecturers or Assistant Lecturers in Biology**

**Qualifications:**

- A minimum GPA of 4.0 in Master of Science or Master of Science with Education in the specified teaching subjects.
- A minimum GPA of 3.5 in Bachelor of Science or Bachelor of Science with Education in the specified teaching subjects
- PhD in Science or Science with Education with a minimum GPA of 4.0 in Master of Science in the specified subjects and a minimum GPA of 3.5 Bachelor of Science or Bachelor of Science with Education in specified subjects.

4. Lecturers or Assistant Lecturers in Law

***Qualifications:***

- A minimum GPA of 4.0 in Master of Laws.
- A minimum GPA of 3.5 in Bachelor of Law
- PhD in Laws with a minimum GPA of 4.0 in Master of Laws and with a minimum GPA of 3.5 Bachelor of Law.

***Job Descriptions & Duties***

Job descriptions and duties will be provided by respective departments after successful interviews and recruitment to the post.

Application letters with the attached CVs, copies of certificates and transcripts have to be sent before **Monday, 4th January 2021 to:**

**THE VICE CHANCELLOR,**
**TUMAINI UNIVERSITY MAKUMIRA, ARUSHA-MOSHI ROAD,**
**P. O. Box 55, USA-RIVER.**

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Maombi yetu kwa Simba, Namungo michuano CAF

**WAWAKILISHI** wa Tanzania Bara kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika, Simba na Namungo watashuka dimbani keshokutwa, Jumatano katika viwanja viwili tofauti kuipeperusha bendera ya nchi katika kinyang'anyiro hicho cha kimataifa kwa ngazi ya klabu.

Katika michuano hiyo yenye utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu barani Afrika, Simba itashuka katika Uwanja wa Taifa wa Zimbabwe kuwakabili wenyeji FC Platinum kwenye mechi ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika. Simba imefika hatua hiyo baada ya kuitoa Plateau United ya Nigeria kwa ushindi wa bao 1-0 ugenini na kutoka sare tasa nyumbani, huku Namungo inayopeperusha bendera ya Tanzania kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, yenyewe ikiitoa Al Rabita FC ya Sudan Kusini kwa jumla ya mabao 3-0.

Endapo Simba itapata matokeo ya jumla katika mechi hiyo na ile ya marudiano itakayopigwa kati ya Januari 5-6, mwakani kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, itafuzu moja kwa moja hatua ya makundi ya michuano hiyo, hivyo kuwa na uhakika wa kuingiza Sh. bilioni 1.2 kutoka kwa waandaaji wa michuano hiyo, Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF) kutokana na kufika hatua hiyo ya makundi. Kwa upande wa Namungo FC, Jumatano itakuwa nyumbani katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam kuikaribisha Al Hilal Obayed ya Sudan katika mechi ya raundi ya kwanza kabla ya timu hizo kurudiana kati ya Januari 5-6, mwakani nchini Sudan. Hata hivyo, endapo Namungo itafanikiwa kuitoa Al Hilal Obayed, bado itakabiliwa na kibarua cha kucheza mechi ya mchujo nyumbani na ugenini dhidi ya timu itakayopangiwa na CAF kutoka zitakazotolewa kwenye raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa, na kama itapata matokeo ya jumla ndipo itakuwa imefuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho.


Hivyo, kinachotakiwa kwa sasa kwa wawakilishi hao wa Tanzania Bara, ni kuhakikisha wanapata ushindi wa kishindo katika mechi zao hizo za awali na kuepuka kutoka sare tasa ili kukwepa kucheza kwa presha katika mechi zijazo za marudiano kwa Simba nyumbani na Namungo ugenini. Ikumbukwe katika mechi ya raundi ya awali, Simba ambayo ilianzia ugenini nchini Nigeria dhidi ya Plateau United, ilifaidia kwa ushindi wake wa bao 1-0, hivyo kuwa na kazi rahisi katika mechi ya marudiano, jambo ambalo inatakiwa tena kuhakikisha inamaliza mchezo mapema keshokutwa, huku ikikwepa kutoka suluhu ili kurahisisha mchezo wa marudiano.

Kikubwa kinachotakiwa katika hatua hii ya mtoano ni timu kuhakikisha inashinda kwa mabao mengi mchezo wa awali, ili kuwa na kazi rahisi kwenye mechi ya marudiano, na kwa timu inayoanzia nyumbani kukwepa sare ya mabao kwani itamfaidisha mpinzani wao wakati zitakaporudiana ugenini. Kwa Namungo ambayo inaanzia nyumbani, njia pekee ni kuhakikisha inamaliza mchezo hapa hapa kwa kupata ushindi wa kishindo, huku ikihakikisha wapinzani wao hawapati bao la ugenini, ambalo linaweza kuwabeba baadaye watakaporudiana. Tunaamini kwa maandalizi yaliyofanywa na yanayoendelea kufanywa na wawakilishi wetu, Simba ikiwa tayari mjini Harare na Namungo ikijichimbia visiwani Zanzibar, yataleta matokeo chanya na kuziwezesha kuendelea kuitangaza Tanzania katika medali ya soka kimataifa. Lakini kwa usajili uliofanywa na timu hizo, ambao umemulika zaidi wachezaji wenye uzoefu mkubwa kwenye michuano ya kimataifa, ni jambo lingine linalotufanya kuamini kwamba kilichobaki ni mashabiki kujitokeza kwa wingi kuzipa sapoti uwanjani ili kuzisaidia kukamilisha malengo yao.

Tunachotamani kuona ni wawakilishi wetu hao wakifuzu na kusonga mbele hatimaye kuiongezea nchi yetu pointi, ili msimu ujao wa michuano hiyo, Tanzania iwe miongoni mwa nchi zitakazoingia jumla ya timu nne kwenye michuano ya kimataifa, na hilo litawezekana tu endapo wachezaji na makocha watatimiza wajibu wao huku mashabiki na Watanzania kwa ujumla bila kujali itikadi zao za kisiasa, imani ama klabu wakiungana kuzisapoti kama mchezaji wa 12 uwanjani. Nipashe tunaungana na Watanzania wote kwa ujumla kuziombea na kuzitakia kila kheri Simba na Namungo katika michuano hiyo ya kimataifa ili ziweze kushinda na kusonga mbele.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



## Simba ikishinda dhidi ya Platinum, Tanzania imeshinda, kila la kheri

Na Adam Fungamwango

**JUMATANO,** wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba, watarusha karata yao ya kwanza ya mkondo wa kwanza wa raundi ya kwanza ya ligi hiyo ngumu barani Afrika kwa ngazi ya klabu.

Simba ipo nchini Zimbabwe kwa sasa, na inatarajia kukutana na timu ngumu ya FC Platinum ya huko ikiwa ni mechi ya kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa kwenye michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika, CAF. Wawakilishi hao wa Tanzania waliingia kwenye raundi ya kwanza baada ya kuitoa timu ngumu ya Plateau ya Nigeria kwenye mechi ya awali.

Kwenye mechi ya kwanza nchini Nigeria, Simba ilishinda bao 1-0, kabla ya kulazimisha suluhu nyumbani na kupita hatua hiyo. Katika mechi ya Jumatano, Simba inatakiwa ifanye vizuri ili ijiweke kwenye mazingira mazuri wakati mchezo wa marudiano nchini Tanzania kati ya Januari 5-6, mwakani.

Kinachotakiwa kwenye mechi hiyo ni Simba kushinda, au kutoka sare ya mabao ili iwe rahisi kumalizia kazi nyumbani. Mara nyingi sare isiyo na mabao ugenini huwa haina faida yoyote, ni kama tu mechi yenyewe haijachezwa na nyumbani inakuwa kama fainali, hivyo wachezaji wanakuwa wakicheza kwa presha zaidi, hasa wakiwa nyumbani mbele ya mashabiki wao.

Kama Simba ikichanga karata zake vizuri ni kwamba hatua ya makundi kwake ni nyeupe, kwa sababu aina ya timu inayocheza nayo si ngumu sana kama ambavyo timu nyingine zilizopita kwenye raundi ya awali zimepangiwa.

Kuna baadhi ya timu ambazo zimepita kwenye raundi hiyo kama Simba, lakini zinakwenda kukutana na vigogo vya soka barani Afrika vikiwamo Al Ahly, TP Mazembe, AS Vita, Zamalek, Mamelodi Sundowns, Raja Casablaca na nyingine.

Mfano mdogo ni timu ya Gor Mahia ambayo iliitoa APR ya Rwanda, inakwenda kukutana na kigogo cha soka Algeria, CR Belouzidad, huku Nkana FC ikienda kukutana na timu ngumu ya Petro de Luanda ya Angola.

Timu nyingi ambazo zilipita kwenye raundi ya mchujo, zimejikuta zikiangukia kwa timu ngumu ambazo zenyewe hazikucheza mechi za awali, badala yake zipo moja kwa moja raundi ya kwanza na zilikuwa zikizisubiri baadhi ya timu kutoka kwenye mchujo.

Na hizi timu mara nyingi ni nadra sana kutolewa kwenye raundi ya kwanza. Zenyewe 'zinaishi' kwenye hatua ya makundi miaka nenda rudi, haijalishi kama zinapata ubingwa, zinafika robo, fainali au nusu.

Na ukiziangalia ndiyo hizo hizo ambazo mara nyingi hugawana ubingwa wa Afrika.

Hapa ni kwamba Simba imefanikiwa kuzikwepa kwenye hatua hii ngumu ya kupigania kuingia makundi na kama kukutana nazo basi iwe huko kwenye makundi. Hii ni faida kubwa kwa Simba, hivyo iitumie bahati hiyo kwa kuitoa FC Platinum kwa sababu si timu ya kutisha kama ambavyo ingeweza kuangukia kwenye mikono ya vigogo vya soka Afrika kama wenzake.

Kama viongozi, benchi la ufundi na wachezaji waliamua kufanya kazi waliotumwa na Watanzania na kuitoa Plateau United, basi hakuna kinachoshindikana kwa FC Platinum. Nilisema kuwa Simba itafute angalau bao moja la ugenini ili liwe na faida kwenye mechi ya nyumbani, lakini ikikwepa kuruhusu kufungwa.

Mwaka jana Simba haikushinda bao lolote nchini Msumbiji dhidi ya UD Songo, tuliona kilichowakuta kwenye mechi ya marudiano kwani licha ya sare ya 1-1 iliondoka kwenye michuano hiyo, lakini bao la ugenini dhidi ya Plateau liliwasaidia.

Kwa sasa michuano hiyo inaonekana kubadilika sana, kwani kwenye mechi zilizopita timu kadhaa ikiwamo Simba, Nkana FC, na Enyimba zilipata ushindi ugenini, lakini zikatoa sare nyumbani. Kwa maana hiyo kumbe inawezekana kabisa Simba kuusaka ushindi Zimbabwe kama ilivyofanya dhidi ya Plateau United, ili kujiweka mazingira mazuri kwenye mechi ya marudiano.

Ikumbukwe pia ushindi wa Simba kama ikiingia makundi kuna asilimia kubwa ya msimu ujao Tanzania ikarejesha nafasi zake nne kama ilivyokuwa msimu uliopita baada ya kufanya vema msimu wa 2018, hivyo Watanzania hawana budi kuiombea iwe na mchezo mzuri ugenini na kuibuka na ushindi dhidi ya FC Platinum.

HABARI KITAIFA

# ‘Walimu/wazazi waadhibiwe udanganyifu wa mitihani’

**Na Rose Jacob,** MWANZA

WADAU wa elimu mkoani Mwanza wameiomba serikali kutoa adhabu kali kwa walimu na wazazi wanaoshirikiana kufanya udanganyifu kwenye mitihani ya taifa.

Wamesema wanafunzi hawana makosa na wala hawastahili kupewa adhabu yanapotokea matatizo ya udanganyifu wa mitihani ya kitaifa.

Akizungumza katika kikao cha mkoa cha uchaguzi wa wanafunzi wanaotarajia kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2021, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi, mkoani Mwanza, Kashinje Machibya, aliomba serikali kuangalia upya sheria husika, ili kumlinda mwanafunzi ambaye hafahamu chochote juu ya njama mbaya za kuiba mitihani.

“Suala la wizi wa mtihani nina imani kubwa mwanafunzi huwa hahusishwi, wahusika ni wakuu wa walimu na wazazi ndiyo wanaotengeneza mchakato hadi suala hilo linafanikiwa, kwa Mwanza ni wanafunzi 84 ndiyo waliofutiwa matokeo hii ni hasara kubwa kwa mtoto aliyehangaika kusoma miaka saba halafu anakuja kuharibiwa na watu wazima kwa maslahi ya shule zao ili zionekane bora katika ufundishaji,” alisema Machibya.

Alisema ni hasara kwa wanafunzi hao, kwa kuwa hawatapata nafasi nyingine ya kusoma katika mfumo rasmi wa elimu nchini.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza, Emmanuel Tutuba, ambaye alikuwa mwenyekiti wa kikao hicho, alisema shule za msingi 968 mkoani hapa zilifanya mtihani, za serikali zikiwa 853 na binafsi 115.

Alisema wanafunzi waliosajiliwa kufanya mtihani mwaka 2020 ni 75,138, wavulana 35,868 na wasichana 39,270, waliofanya mtihani ni watahiniwa 74,160, wavulana ni 35,445 na wasichana 38,705 sawa na asilimia 98.7 ya wanafunzi wote.

“Wanafunzi waliofaulu mtihani huo ni 64,422 kati ya 74,160 waliofanya mtihani, 978 hawakufanya mtihani huo kwa sababu mbalimbali zikiwamo utoro, ugonjwa, mimba na vifo, wavulana 446 na wasichana 532 sawa na asilimia mbili,” alisema Emmanuel.

Emmanuel alisema wanafunzi 84 waliofutiwa matokeo ni wa Halmashauri za Misungwi, Ilemela, Buchosa na Sengerema na ufaulu wa mkoa katika mtihani wa darasa la saba 2020 umepanda kutoka asilimia 83.93 hadi asilimia 86.71.

“Kuzuiliwa kwa awali kwa matokeo wanafunzi 45 wa Shule ya Msingi Kwezi kutokana na kutolipa ada ya mtihani katika Baraza la Mitihani la Taifa (NACTE), kumeathiri ufaulu wa mkoa.

# Miradi ya kimkakati nchini yaikosha EAC

**Na Mwandishi Wetu**

JUMUIYA ya Afrika Mashariki (EAC) imeeleza kuvutiwa na miradi mikubwa na ya kimkakati inayotekelezwa na Tanzania, na kwamba kukamilika kwake kutachochea ukuaji wa uchumi na biashara katika jumuiya hiyo.

Aidha, jumuiya hiyo imeeleza kuwa miradi hiyo itarahisisha huduma za usafiri na usafirishaji.

Aliyebainisha hayo ni Naibu Katibu Mkuu wa Sekretarieti ya EAC (anayeshughulikia masuala ya Mipango, Miundombinu, Fedha na Utawala), Steven Mlote, ambaye aliongozana na ujumbe wa jumuiya hiyo walipotembelea mradi wa ujenzi wa bwawa la kufua umeme la Julius Nyerere ambalo linatarajiwa kukamilika Juni 2022 ambalo litazalisha migawati 2,115 za umeme.

Mlote alieleza kuvutiwa na taarifa ya mradi huo kufadhiliwa na fedha za Watanzania, na kumpongeza Rais John Magufuli kwa maono hayo, lakini kitendo cha kutoa zaidi ya ajira 5,000 ambapo asilimia 90 ni Watanzania.

Awali ujumbe huo ulitembelea mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kwa lengo la kijionea maendeleo ya ujenzi wa maradi huo, na kueleza kufurahishwa na kazi kubwa inayofanywa na Serikali ya Tanzania.

Ujumbe huo uliwasihi vijana wa Kitanzania waliopata fursa ya ujenzi wa reli kuendelea kujifunza kwa moyo na kwa kujituma ili kupata maarifa na ujuzi wa kuendelea kutunza, kuendesha na kuendeleza mradi huo hata baada ya wataalamu kutoka kampuni inayohusika na ujenzi kuondoka nchi.

Mlote alitoa wito kwa Watanzania hasa ambao wanazunguka eneo la miradi hiyo kuitunza na kuilinda kwa kuwa manufaa yake ni pamoja na kuongeza uzalishaji wa mazao mashambani na bidhaa za viwandani pia kurahisisha usafirishaji wa bidhaa na watu katika za EAC.

The Guardian www.ippmedia.com
Nipashe MWANGA WA JAMII




For our Advertisement Customers

| Just pay for your Print advertisement | Get Free | | | |
|---|---|---|---|---|
| Size of Advertisement | Free E-Paper for One Month | | Free Social Media Post | |
| | The Guardian | Nipashe | Guardian or Nipashe | Guardian or Nipashe |
| Full Page | 10 E-Papers | 10 E- papers | 5 Posts | 5 Posts |
| 3/4 Page | 7 E- Papers | 7 E - Papers | 2 Posts | 2 Posts |
| 1/2 Page | 5 E- Papers | 5 E- papers | 2 Posts | 2 Posts |
| 3/8 Page | 3 E- Papers | 3 E- Papers | 1 Post | 1 Post |
| 1/4 Page | 2 E- Papers | 2 E- Papers | 1 Post | 1 Post |




For More Information Please Contact us:
0782 253 676 advertise@guardian.co.tz

1. This offer is Valid till 31st Dec 2020
2. Terms and conditions apply

# Wanafunzi UDSM wadhaminiwa masomo ya takwimu za Ukimwi

**Na Christina Mwakangale**

WANAFUNZI watano katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Shule ya Teknolojia Habari na Mawasiliano (COICT), wamepata udhamini wa masomo ya Shahada ya Uzamili wa Sayansi ya Data, ili kufanikisha ukusanyaji wa takwimu kuhusu Virusi Vya Ukimwi (VVU) na Ukimwi.

Udhamini huo wa miaka miwili, umetolewa na Tanzania Data Lab (dLab), Data Collaborative for Local Impact (DCLI) kwa kushirikiana na mradi wa President's Emergency Plan for AIDS Relief (PEPFAR) kutoka Serikali ya Marekani.

Mhadhiri wa chuo hicho, Idara ya Sayansi ya Kompyuta na Uhandisi, Dk. Ellen Kalinga, akizungumza mwishoni mwa wiki, baada ya kuwakabidhi vyeti wanafunzi hao, alisema matarajio ni wanafunzi hao kufanya vizuri katika masomo na kusaidia maambukizi kupungua.

"Hii ni awamu ya tatu kundi la wanafunzi kudhaminiwa na mradi huu, tunategemea wawe wataalamu katika kutumia takwimu hasa katika Ukimwi, VVU... chuo kazi yetu ni kutoa watu wanaokuja kutatua matatizo kwenye jamii," alisema Dk. Kalinga.

Alisema lengo la PEPFAR kudhamini shahada hiyo ni kuwa na kituo kimoja cha takwimu kuhusu Ukimwi, kufanya utafiti na kusaidia kutoa mwongozi kwa watunga sera.

Dk. Kalinga alisema mradi huo umesaidia katika elimu kwa wanafunzi wa elimu ya juu, kuwajengea uwezo katika masuala ya takwimu na kupunguza maambukizi.

"Mliopata udhamini huu msituangushe chuo, mmepata fursa kati ya waliiomba 22, kuna takwimu ambazo hazijakusanywa pamoja kuhusu Ukimwi, mkawe wafumbuzi katika suala hili," alisema Dk. Kalinga.

Mkurugenzi Mkuu wa Tanzania Data Lab,(dLab), Stephen Chacha, alisema mchakato wa kupata udhamini wa masomo hayo ulianza kwa waombaji 22 kutuma maombi, kisha mchujo wa ushindani kufanyika na kuwapata watano kati ya hao.

Chacha alisema waliopata udhamini miongoni mwa wanawake ni wawili, na kwamba hatua hiyo inatokana ushirikiano mzuri uliipo baina ya UDSM Idara ya COICT na dLab.

"Udhamini huu unafanya jumla walioingia katika mpango huu kufikia 14 chini ya Data Collaboratives for Local Impact (DCLI) na dLab kupitia PEPFAR, kuwezesha vijana wa Tanzania kuwa wataalamu katika sayansi ya takwimu," alisema Chacha.

Alisema takwimu zimeleta mapinduzi na kufanya mahitaji kuongezeka hususan kwa wanasayansi nchini na duniani. "Wanasayansi wanatarajia kutumia ujuzi zaidi kupitia takwimu ili kukabiliana na maambukizi ya VVU na Ukimwi," alisema Chacha na kuongeza: "Mfano nusu ya Watanzania wanaoishi na Ukimwi hawajui hali zao, matumaini yetu ni kuwa wanafunzi hawa watatafuta mbinu na kubuni njia sahihi kuhusu hili na huduma kwa kundi hili."

"Tangu kuanzishwa kwa PEPFAR nchini mwaka 2003 vifo vitokanavyo na Ukimwi vilipungua kwa asilimia 70 na kuzuia maambukizi mapya milioni 1.1 na vifo 690,000.

Mabadiliko haya yanatokana na umuhimu wa takwimu kwa wataalamu wa afya na jamii ili kuwa na kizazi kisicho na maambukizi," alisema Chacha.




# Waziri aipa mtihani TIC uzalishaji ajira milioni 8

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais (Uwekezaji), Prof. Kitila Mkumbo, amekitaka Kituo cha Uwekezaji (TIC) kuwa chachu ya kufikia malengo ya serikali ya kufikia asilimia 8 ya pato la taifa sambamba na kuzalisha ajira milioni 8 katika kipindi hiki cha awamu ya pili ya uongozi wa Rais John Magufuli.

Prof. Mkumbo alitoa agizo hilo katika kikao na menejimenti na wafanyakazi wa kituo hicho jijini Dar es Salaam, baada ya kufanya ziara yake ya kwanza tangu kuteuliwa kushika wadhifa huo, na kusema TIC ina jukumu kubwa kuhakikisha wanavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza nchini, ili kufikia malengo ya serikali ya kujenga uchumi wa viwanda ifikapo 2025.

"Malengo ya serikali ni kufikia asilimia 8 ya pato la taifa na kuhakikisha uchumi wetu unazalisha ajira milioni 8, hivyo kila mtumishi ana wajibu wa kutekeleza majukumu yake, ili malengo yaweze kutekelezeka na kuifanya nchi yetu kuwa na maendeleo endelevu," alisema Prof. Mkumbo

Alieleza kuwa TIC iwe mwezeshaji katika kurahisisha usajili wa miradi mbalimbali ya wawekezaji jambo litakalovutia zaidi wawekezaji kuja Tanzania na kufanya uwekezaji kupitia fursa mbalimbali zilizopo.

"Tanzania ipo katika mazingira mazuri ya kuvutia uwekezaji ikiwa ni pamoja utulivu wa kisiasa, maboresho ya sera, sheria na kanuni za uwekezaji pamoja na uhakika wa soko kutokana na nchi kuwa mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini wa Afrika (SADC) ni sehemu ya vivutio," alisema Prof. Mkumbo.

Aliongezea kuwa maboresho ya mifumo ya elimu yamepelekea kuwapo kwa wafanyakazi wenye weledi pamoja na gharama za nguvukazi kuwa rafiki ni sehemu ya mazingira wezeshi kwa wawekezaji kuvutiwa kuwekeza, hviyo ni jukumu la TIC katika kujipambanua kwa wawekezaji ndani na nje ya nchi ili waweze kupata taarifa. Katika hatua nyingine, Prof. Mkumbo ameitaka TIC kuimarisha uratibu wa mahusiano na taasisi nyingine za serikali ili utoaji wa huduma za usajili wa miradi ya wawekezaji ifanyike kwa urahisi pasipo na vikwazo vyovyote, hali itakayoiweka Tanzania kwenye nafasi za juu kwenye orodha ya nchi zenye mazingira wezeshi ya uwekezaji duniani.

"Muhimu kwa mamlaka zetu kuwa na utaratibu maalum wa kwenda kufanya ukaguzi kwa wakati mmoja, ili kupunguza muda wa ukaguzi wa mara kwa mara kwa kila taasisi jambo linalokwamisha uzalishaji, hivyo tukiboresha hili tutazidi kujiweka kwenye mazingira mazuri ya kuchochea uwekezaji," alisema Prof. Mkumbo.

Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, Dk. Maduhu Kazi, alimshukuru waziri kwa kutembelea ofisi yake na kutoa maagizo mbalimbali hususani suala la kujitangaza ndani na nje ya nchi juu ya kuvutia wawekezaji.

HABARI KITAIFA

# Wavuvi watakiwa kuzingatia sheria

Na Sabato Kasika

WAVUVI wa mialo ya Busekera, Bwai Kumsoma, visiwa, Iriga na Rukuba, Wilaya Musoma mkoani Mara, wametakiwa kuzingatia sheria, taratibu na kanuni zinazosimamia uvunaji wa rasilimali za ziwa.

Hayo yalisemwa na Ofisa Uvuvi wa Halmashauri ya Musoma, Augustine Costantine, katika ziara ya viongozi wa halmashauri hiyo ya kutembelea wavuvi wa maeneo hayo yenye lengo la kuboresha shughuli za wavuzi.

Miongoni mwao ni Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Musoma, Tanna Nyabange, msaidizi wake Nyanjara Majura na viongozi wa Benki ya Equity ambao walihamasisha wavuvi kujiunga na benki hiyo.

Ofisa uvuvi alisema, ni muhimu wavuvi wabadilike na wazingatie sheria, taratibu na kanuni, kwa kuachana na matumizi ya nyavu haramu, na kwamba kila mvuvi awe mlinzi na mwalimu wa mwenzake.

"Umefika wakati nyie wavuvi wenyewe mkomeshe uvuvi haramu, kwa kuzingatia sheria, taratibu na kanuni, hasa kuepuka matumizi ya nyavu mbazo zimepigwa marufuku," alisema Costantine.

Alisema halmashauri itaendelea kutoa elimu kwa wavuvi ili maeneo yote ya uvuvi yaendelee kuwa salama na kuwataka wavuvi kutambua umuhimu wa elimu hiyo ili kuepuka kuingia kwenye hatia.

Naye Ofisa Maendeleo ya Jamii, Tanna Nyabange, aliwataka waavuvi kujiunga katika vikundi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na pia kupata mikopo kutoka Halmashauri ya Musoma na taasisi nyingine za fedha. Aidha, katika ziara hiyo ya kutembelea wavuvi hao, viongozi wa Benki ya Equity nao walikuwapo wakihamasisha wavuvi kujiunga na benki hiyo waweze kupata mikopo ya kuboreshea shughuli zao.

Mmoja wa viongozi hao, Kemilembe Kabugumila, alisema, wamefanikiwa kuandikisha vikundi 79 vyenye wanachama 1035, ambavyo benki hiyo itaanza navyo katika utoaji wa mikopo.

"Kabla ya yote, sisi maofisa wa Benki ya Equity tutaonana kwanza na Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vincent Anney na Mbunge Prof. Sospeter Muhongo kujadili fursa ya upatikanaji wa mikopo kwa vikundi vya wavuvi wa Musoma Vijijini," alisema Kabugumila.

Kabugumila alisema benki hiyo iko tayari kutoa mikopo kwa vikundi vya wavuvi, na kwamba matayarisho yanaendelea, ikiwamo kuonana kwanza na mkuu wa wilaya na mbunge kuweka mikakati ya kufanikisha jambo hilo.


## NOTISI / TANGAZO

**(MAREKEBISHO YA TANGAZO LA GAZETI LILITOKA TAREHE 15/12/2020 ISSN NO. 0856 Na. 0580430)**

**CHAMPION AUCTION MART LTD, SUNDI AUCTION MART LTD, SMARKCORE GROUP LTD, NUTMEG AUCTIONEERS AND PROPERTY MANAGERS CO.LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, MASETO AUCTIONEERS AND DEBT COLLECTORS LTD,BEST GROUP LTD SALEI AUCTION MART LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya benki ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili. Vinginevyo, tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha

| S/N | JINA LA MTEJA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | JOHN JOSEPH NYAMGINI | JOHN JOSEPH NYAMGINI | NYUMBA | NYAMUHONGOLO-MWANZA | 05/01/2021 NAKUENDELEA |
| 2 | WANJERU CONSTRUCTION CO. LTD | IDD MOHAMED | TITTLE NO. 23519, L.O NO. 1338 BLOCK 'M' | PASIANSI-MWANZA | 30/12/2020 NAKUENDELEA |
| 3 | LWEYEMAM MEDARD KABENDERA | LWEYEMAM MEDARD KABENDERA | TITTLE NO. 74288, L.O NO 542135, PLOT NO. 318, BLOCK 'A' | NYASHISHI | 30/12/2020 NAKUENDELEA |
| 4 | RENATUS CHRISTIAN PETRO | RENATUS CHRISTIAN PETRO | KIWANJA | MIGANGA KATA YA MKONTHE-DODOMA | 30/12/2020 NAKUENDELEA |
| 5. | VICTOR MOSSES NNKO | VICTOR MOSSES NNKO | NYUMBA | KIBAIGWA MTAA WA MAJENGO-DODOMA | 02/01/2021 NAKUENDELEA |
| 6. | RUTTA GODFREY RWECHUNGURA | RUTTA GODFREY RWECHUNGURA | KIWANJA TITTLE NO. 48395-DLR | MTAA WA MATHIAS KATA YA MIYUJI-DODOMA | 30/12/2020 NAKUENDELEA |
| 7. | TITO KALAM SANGA | TITO KALAM SANGA | NYUMBA | KITONGOJI CHA KARUME-KIBAIGWA-DODOMA | 02/01/2021 NAKUENDELEA |
| 8. | JULIUS KALANGA LAIZER | JULIUS KALANGA LAIZER | PLOT NO. 802 & 803, BLOCK 'N' | MJI MPYA STREET – MONDULI -ARUSHA | 30/12/2020 NAKUENDELEA |
| 9. | PATRICK OMBENI LEMA | PATRICK OMBENI LEMA | PAGARE LA NYUMBA | MTAA NDACHI NDACHI KATA YA MNADANI | 30/12/2020 NAKUENDELEA |
| 9. | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | NAMBA YA HATI -46357 MBYLR,L..O NO. 505295, L.D NO. – TDM/4481PLOT NO. 54 & 55,KITALU NA. C | TUNDUMA | 30/12/2020 NAKUENDELEA |
| | | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | NAMBA YA HATI ;47332-MBYLR,L.O.NO.788027,KIWANJA NO. 160,KITALU NA;N | MBEYA | 30/12/2020 NAKUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika. Na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. 0754 497 396 / 0752 000 695
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA

WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI

BRELA
BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY

## TAARIFA KWA UMMA

### TAHADHARI KWA TAASISI ZA SERIKALI, BINAFSI NA UMMA KUHUSU MAKAMPUNI AMBAYO HAYAJAHUISHA (UPDATE) TAARIFA ZAKE KWA MUJIBU WA SHERIA

**Dar es Salaam, Desemba 19, 2020**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) unapenda kutoa tahadhari kwa Wizara, Mamlaka, Taasisi za Serikali, Taasisi Binafsi na Umma kwa ujumla kuhusu uwepo wa Makampuni ambayo hayajahuisha (update) taarifa zake kwa Mujibu wa Sheria.

Kwa taarifa hii, Umma unahimizwa kuhakikisha Mikataba yote ya manunuzi ya vifaa au huduma ***(All kinds of contractual transactions)*** baina yao na Kampuni binafsi isainiwe baada ya kujiridhisha kwamba Kampuni husika imehuisha taarifa zake za mwaka katika Daftari la Makampuni kama yalivyo matakwa ya Sheria na kama kampuni hizo bado ziko hai. Kujiridhisha huko kufanyike kwa Kampuni husika kutakiwa kuwasilisha Cheti cha Usajili (Certificate of Incorparation) na nakala ya Mizania yake ya Mwaka huo (Annual returns) iliyoidhinishwa na Msajili wa Makampuni au Taarifa Rasmi (Official Search Report) iliyosainiwa na Msajili wa Makampuni.

BRELA inapenda kukumbusha Umma kuwa, kwa mujibu wa kifungu cha 128 cha Sheria ya Makampuni, Sura 212 kila Kampuni iliyosajiliwa hapa nchini (Locally Registered Company) inapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Makampuni Taarifa za Mwaka (Annual Returns) na kwa upande wa Kampuni zilizosajiliwa nje ya nchi (Companies incorporated outside Tanzania) na kufungua tawi hapa nchini, huwasilisha Mahesabu ya Mwaka (Annual Accounts) kwa mujibu wa kifungu cha 438 cha Sheria ya Makampuni, Sura 212.

Izingatiwe kwamba, Taarifa ya mwaka husaidia kutoa taswira halisi ya Kampuni na hivyo kusaidia mtu yeyote anayetaka kuingia makubaliano ya kibiashara na Kampuni husika kufanya maamuzi stahiki na kufahamu ni nani haswa wanahusika na utiaji saini wa mikataba.

BRELA inatoa rai kwa Wizara, Mamlaka, Taasisi za Serikali, Taasisi Binafsi na Umma kwa ujumla kuchukua tahadhari dhidi ya kampuni ambazo hazija huisha taarifa zake kwa mujibu wa Sheria, hii itasaidia kuepusha madhara ya kisheria na kiuchumi yanayoweza kujitokeza kwa kufanya kazi na kampuni ambayo haijahuisha taarifa zake kwa Msajili wa Makampuni.

***"Tunaipa utu wa kisheria biashara yako"***

**Imetolewa na:**

**AFISA MTENDAJI MKUU**

**WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI**




Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi Benki ya NMB, Margareth Ikongo, akimvalisha kofia mmoja wa wahitimu katika programu ya mafunzo ya uongozi ya mwaka 2018-20202 ya Benki ya NMB. Kulia ni Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa benki hiyo, Filbert Mponzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ofisa ardhi ahukumiwa kwa kughushi nyaraka

**Na Happy Severine,** MASWA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu, imemhukumu aliyekuwa ofisa ardhi wa wilaya hiyo, Octavian Mishana, kwenda jela miaka mitano au kulipa faini ya Sh. 600,000 kwa kosa la kughushi nyaraka.

Hukumu hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Enos Misana, baada ya mshtakiwa kukiri kosa linalomkabili.

Baada ya mshtakiwa kukiri makosa yake Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Rehema Sakafu, aliiomba mahakama hiyo kutoa adhabu kwa mshtakiwa ili liwe fundisho kwa watu wengine wenye tabia kama hiyo.

Kabla ya mahakama kutoa hukumu hiyo, mshtakiwa aliiomba mahakama impunguzie adhabu kwa kuwa ana umri mkubwa, anaumwa kisukari na ni kosa lake la kwanza.

Awali ilidaiwa na mwendesha mashtaka kuwa mshtakiwa alifikishwa mahakamani hapo Septemba 19, mwaka 2019 kwa kosa la kughushi stakabadhi ambazo alidai ni za halmashauri hiyo, huku akifahamu si kweli na kukusanya Sh. 1, 192,000 kwa ajili ya kupima viwanja badala yake akazitumia kwa matumizi yake binafsi.

Mwendesha mashtaka alieleza mahakama kwamba mshtakiwa alitenda kosa hilo kati ya mwaka 2002 hadi 2007 akiwa Ofisa ardhi wa wilaya hiyo kabla ya kuhamishiwa Biharamulo mkoani Kagera ambapo kwa sasa amestaafu kazi serikalini.

Mshtakiwa alilipa faini hiyo na kukwepa kwenda jela na hivyo kuachiwa huru.

# Mbunge atwishwa kero ya stendi

**Na Sabato Kasika**

WATUMIAJI wa stendi mpya ya mabasi ya mjini Nachingwea mkoani Lindi wakiwamo abiria na wafanyabiashara wadogo, wamelalamikia kero mbalimbali wanazokumbana nazo katika stendi hiyo na kuomba zitatuliwe.

Miongoni mwa kero hizo ni kukithiri kwa vumbi, kutokana na kuwapo kwa udongo wa tifutifu, jambo ambalo ni hatari kwa afya zao, uchache wa vyoo na mazingira duni ya kufanyia biashara.

Walitoa kero hizo juzi, mbele ya Mbunge wa Nachingwea, Dk. Amandus Chinguile, alipotembelea stendi hiyo ili kujua kero zinazowakabili watumiaji wa stendi hiyo wakiwamo pia madereva na makondakta.

Moja ya kero ambazo walimweleza mbunge huyo ni kuwapo kwa choo chenye matundu mawili ambayo wamedai hakitoshi kulingana na wingi wa watu na kuomba viongezwe vingine angalau kufikia matundu sita.

"Huduma ya choo ni ya muhimu sana mheshimiwa, tunaomba uwasiliane na watu wa halmashauri walione tatizo hili na kulifanyia kazi," alisema mmoja wa watumiaji wa stendi hiyo aliyejitambulisha kwa jina la Juma Nanji.

Mamalishe aliyejitambulisha kwa jina la Mwajuma Shaban, aliomba stendi hiyo ijengwe mabada ya kisasa ya biashara ili kuvutia wateja zaidi badala ya ilivyo sasa akidai yaliyopo ni ya kienyeji.

"Si hilo tu bali stendi ina vumbi jingi sana ambalo ni hatari kwa afya zetu wafanyabiashara, wateja na abiria, hivyo tunaomba hili nalo lifanyiwe kazi kwa ualama wa afya zetu," alisema Mwajuma.

Naye abiria aliyejitambulisha kwa jina la Abubakar Saleh, alisema stendi kuwa na geti moja ni kero, kwa madai kwamba linasababisha abiria wanazunguka na umbali mrefu kuingia ndani, na aliomba yaongezwe mageti mawili katika maeneo mengine ya ukuta wa stendi hiyo.

Akijibu kero hizo, mbunge huyo aliahidi kuzifanyia kazi kwa kuwasiliana na uongozi wa halmashauri ya Nachingwea, huku akisema ataendelea kuwa karibu nao ili kusaidiana kuleta maendeleo.

Mbunge huyo aliwataka kila mmoja kuendelea na shughuli zake kama kawaida wakati yeye akiwasiliana na mamlaka husika ili kumaliza kero zilizopo kwenye stendi hiyo iliopo nje kidogo ya mji wa Nachingwea.

"Lengo la ziara yangu lilikuwa ni kutambua kero mbalimbali katika eneo hili la stendi, mmeziweka wazi, na mimi ninazichukua kuzipeleka mahali husika ili zifanyiwe kazi," alisema Dk. Chinguile.

# Mafunzo kazini yazalisha ajira 50 Benki NMB

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imefanikiwa kutengeneza fursa za ajira kwa wahitimu wa vyuo vikuu zaidi ya 50 kupitia programu yake maalumu ya mafunzo ya vitendo kazini iliyoanzishwa takribani miaka 10 iliyopita.

Mbali na kutoa fursa kwa wahitimu wasio na kazi na sifa zinazohitajika kuajiriwa moja kwa moja, uwekezaji huo umeiwezesha NMB kuzalisha wafanyakazi wenye ujuzi na weledi mkubwa katika masuala ya kifedha na kibenki.

Akizungumza wakati wa mahafali ya wahitimu watano wa mwaka huu wa programu hiyo, Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa NMB, Filbert Mponzi, alisema mchakato huo si muhimu tu kwa benki hiyo na washiriki wake bali pia kwa tasnia ya fedha na nchi kwa ujumla.

Mahafali hayo yalifanyika Ijumaa makao makuu ya NMB jijini Dar es Salaam na tayari zoezi la kupata wanafunzi wengine 10 watakaoanza mafunzo hayo mapema mwakani yanayochukua miaka miwili limekamilika.

"Tunalo lengo la kutatua changamoto mbalimbali zinazowakumba vijana hususani kwenye masuala ya ajira nchini, hivyo vijana hawa tuliwachukua walivyomaliza kozi mbalimbali vyuoni na kuwapa ujuzi katika maeneo ya kazi ili waweze kuwa na uzoefu wanapoajiriwa," Mponzi alifafanua.

Kwa niaba ya Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, Mponzi aliwataka wahitimu hao kuitendea haki imani ya benki hiyo kwao na kuwa wafanyakazi bora na waadilifu. Pia aliwaomba kuitumia nafasi hiyo adimu waliyopata kuisogeza NMB mbali zaidi kimafanikio na kuisaidia kuendelea kutoa huduma bora.

Ngeni rasmi katika mahafali hayo alikuwa Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa NMB, Margaret Ikongo, aliwapongeza wahitimu kwa kuzishinda changamoto walizokumbana nazo baada ya masomo vyuoni.

Alisema hiyo ni mojawapo ya sababu zilizochangia utendaji wao bora na ufanisi kazini mpaka kuajiriwa moja kwa moja na NMB. "Jinsi mlivyofanya kazi kwa bidii, uvumilivu, juhudi, maarifa, nidhamu na kujituma kipindi cha mafunzo ya miaka miwili, naomba msiishie hapa tu, bali muende mkalete mapinduzi kwenye kila kazi mnayogusa ili benki yetu iendelee kusonga mbele," alisema Ikongo.

Akizungumza kwa niaba ya wahitimu wenzake, Agnes Nyanzala, alieleza kuyafurahia mafunzo ya vitendo kwa miaka miwili, yaliyojaa uwezeshaji uliowapa urahisi wa kiutendaji, kiasi cha kuivutia NMB na kuwapa ajira.

Nyanzala alisema kwa sasa wameiva vya kutosha na wana ari kubwa katika kufanya kazi kwa bidii, maarifa na weledi na kwamba wako tayari kwa mamapambano ya kunyanyua ustawi wa NMB kuanzia mwaka ujao wa 2021.

Programu ya mafunzo kazini ya NMB ilianzishwa mwaka 2009 na kila baada ya miaka miwili benki hiyo uwatuma wataalamu wake wa rasilimali watu kwenda vyouni kutafuta wanafunzi wenye vipaji wapate mafunzo ya vitendo ndani ya benki.

Nipashe
Spotika



NYOTA WA5 WA KUSAJILIWA BARCA KUMBAKISHA MESSI UK. 12&13




Aubameyang Ozil Lacazette

# SABABU 5 ARSENAL YA ARTETA INAPATA TABU

**LONDON, England**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta aliwahi pale London Kaskazini kwa ajili ya kuimarisha timu kuwa ya ushindani. Ingawa klabu haikuweza kumaliza kwenye nne bora na kurudi Ligi ya Mabingwa Ulaya, vijana hao wa Arteta walinyanyua taji la FA kwa kuwafunga Manchester City na Chelsea kwenye mechi mfululizo.

Klabu hiyo ilianza msimu wa 2020-21 vizuri kwa kuwafunga mabingwa watetezi wa Ligi Kuu England, Liverpool kwenye mchezo wa Ngao ya Jamii.

Ushindi wa 3-0 dhidi ya Fulham ukafuata kwenye mchezo wa ufunguzi wa msimu, Arsenal ikapaa kileleni mwa msimamo baada ya kuibuka na ushindi wa 2-1 dhidi ya West Ham nyumbani.

Hata hivyo, mambo yakabadilika haraka Arsenal ikajikuta ikipoteza mechi zake nane kati ya 14 za Ligi Kuu na kujikuta kwenye nafasi ya 15 katika msimamo.

'Washikabunduki' hao kwa sasa wamekuwa na wakati mgumu zaidi, ambapo mchezo wao wa mwisho walicheze kichapo cha mabao 2-1 mwishoni mwa wiki kutoka kwa Everton.

Licha ya kuanza vizuri kwa kocha Arteta, Arsenal sasa hali ni mbaya.

Makala haya yanakuchambulia sababu tano kwa nini kikosi cha Arsenal kinapata tabu sana chini ya Arteta ambaye ni raia wa Hispania, hizi hapa...

**#1. Kumbadilisha nafasi Aubameyang**

Baada ya kuwasili Arsenal mwaka 2018, Pierre-Emerick Aubameyang alikuwa na kiwango cha kuvutia akifunga mabao 70 katika mechi 109 kwenye mashindano yote kabla ya msimu huu.

Nyota huyo wa zamani wa Borussia Dortmund, alikuwa mfungaji bora wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, msimu wa 2016-17, akarudia msimu wa 2018-19 kwenye Ligi Kuu England. Aubameyang alifurahia tena mabao 22 msimu uliopita.

Mabao mawili katika mechi 12 za Ligi Kuu msimu huu yameifanya Arsenal kuwa kwenye kiwango kibovu kabisa. Arteta amembadilisha kutoka nafasi aliyozoea kucheza Aubameyang ya mshambuliaji wa kati na kumuweka kama winga mchezaji huyo wa kimataifa wa Gabon.

Aubameyang mara kwa mara ameonekana kuwa peke yake huku akihitaji kurudi kucheza kwenye nafasi aliyoizoea na kupata mipira ya kutosha. Kama hilo litatokea, straika huyo anaweza kufunga mabao mengi zaidi na Arsenal itarudi kwenye nafasi yake.

**#2. Kukosekana kwa mabao**

Huku straika wao, Aubameyang akiwa hafungi kabisa mabao pale mbele, Arsenal imefunga mabao 11 katika mechi 12 za Ligi Kuu msimu huu.

Kushindwa kwa 'Washikabunduki' hao kufunga umekuwa mwanzo mbaya zaidi tangu msimu wa 1981-82 walipokuwa kwenye wakati kama huu.

Lakini pia wachezaji kama Alexandre Lacazette na Willian wameshindwa kumlisha mipira Aubameyang pale mbele, ndio sababu kubwa ya Arsenal kushindwa kufunga.

Willian amekuwa na kiwango duni tangu alipotua Arsenal kipindi cha majira ya joto kilichopita.

**#3. Kutemwa kwa Ozil**

Mesut Ozil ametemwa kwenye kikosi cha Arsenal tangu Machi mwaka huu. Wakati ni ukweli kwamba kiungo huyo wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 32 ,alikuwa bora zaidi, bado ana nafasi ya kuendelea kucheza kwa kiwango cha juu kwa miaka michache ijayo.

Uamuzi wa kumuondoa Ozil kutoka kikosi cha Arsenal kwenye Ligi Kuu kinaonekana wazi kuwa safu ya kiungo imekosa mtu mbunifu, kwani Joe Willock na Lacazette wameshindwa kupandisha mashambulizi.

Ni wazi kabisa Arteta anahitaji huduma ya Ozil pale kati ili kuweza kuchangamsha mashambulizi kwenda mbele.

Kwa kushindwa kumtumia Ozil, Arteta atakuwa na kazi ngumu mno ya kupata mtu wa kuunganisha kiungo na safu ya ushambuliaji.

Hata kocha wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger amenukuliwa akisema Ozil bado ana nafasi kwenye kikosi cha kwanza cha Arsenal.

**#4. Mfumo wa ulinzi wa Arteta**

Muda mrefu umepita tagu Arsenal ilipokuwa ikitumia zaidi walinzi wa pembeni kupandisha mashambulizi.

Chini ya Arteta kwenye Ligi Kuu msimu huu, Arsenal imeshindwa kupata matokeo mazuri kwa sababu ya mfumo wake wa ulinzi. Na hilo ndio limechangia kwa viungo kushindwa kuwalisha mipira Aubameyang au Lacazette.

**#5. Hali ya William Saliba**

Baada ya kupelekwa kwa mkopo wa muda mrefu kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, William Saliba alichukuliwa kama ndiye mchezaji muhimu zaidi kwa Arsenal msimu huu. Lakini mambo yamekuwa tofauti.

Mlinzi huyo wa zamani wa Saint Etienne bado hajaanza kuichezea Arsenal licha ya 'Washukabunduki' hao kutokuwa na Sokratis Papasthatopoulos mwenye uzoefu kwenye kikosi chake kwa msimu huu.

Kocha wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho anamlinganisha Saliba na Kurt Zouma, huku mchezaji wa zamani wa Liverpool, Jimmy Carragher akishangaa kwa nini Arteta hamchezeshi Saliba.

**ISIKUPITE**

BAO la kusawazisha alilofunga Lionel Messi wakati wakitoka sare ya 2-2 dhidi ya Valencia kwenye LaLiga juzi, linamfanya straika huyo wa Barcelona na Argentina kuifikia rekodi ya nguli wa Brazil, Pele, ya kufunga mabao 643 kwa klabu moja. Pele alifunga mabao 643 katika misimu 19 aliyoitumikia klabu ya Santos ya Brazil kati ya mwaka 1956 na 1974.



## Extra Time

# NYOTA WA5 WA KUSAJILIWA BARCA KUMBAKISHA MESSI



Sergio Ramos

Neymar

**BARCELONA, Hispania**

BAADA ya Barcelona kumaliza msimu uliopita bila taji lolote kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha zaidi ya muongo mmoja, huku wakikutana na kichapo cha mabao 8-2 kutoka kwa Bayern Munich kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, Lionel Messi aliwasilisha maombi ya kutaka kuondoka klabuni hapo.

Hata hivyo, mwisho wa siku Messi aliamua kubakia klabuni hapo ili kumalizia mkataba wake ambao unamalizika mwishoni mwa msimu huu.

Barcelona bado inaendelea na jitihada za kuhakikisha Messi ambaye tangu utoto wake amekuwa akicheza kwenye klabu hiyo, kumbakiza na kuendelea kukipiga pake Camp Nou.

Katika jitihada hizo, wagombea kadhaa wa urais wa klabu hiyo wamekuwa wakitoa kauli ya kutaka kumbakiza nyota huyo kwa namna yoyote ile.

Uchaguzi wa urais wa klabu hiyo unatarajiwa kufanyika Januari 24, mwaka huu.

Katika kuhakikisha hilo, makala haya yanakuchambulia wachezaji watano ambao wanaweza kusajiliwa Barcelona kwa ajili ya kumshawishi Messi asiondoke, ambao ni hawa hapa...

**#5. Luis Suarez**

Usajili huu unaweza kuonekana usiowezekana kwa wakati huu, lakini Barcelona wanaweza kuangalia namna ya kumrudisha Luis Suarez pale Camp Nou kipindi kijacho cha majira ya joto baada ya raia huyo wa Uruguay kwenda kule Atletico Madrid.

Straika huyo mwenye umri wa miaka 33, amekuwa na mwanzo mzuri kule 'Rojiblancos', akifunga mabao saba kwenye mechi tisa za LaLiga.

Kama ataendelea na kiwango chake hicho kizuri kwa msimu wote, anaweza kuisaidia Atletico kushinda taji lake la kwanza la LaLiga kwa kipindi cha miaka sita, na Barcelona wanaweza kufikiria kumuunganisha tena Suarez na Messi msimu ujao.

Kwa kipindi chake alichocheza pale Barcelona, Suarez alifunga mabao zaidi ya 200 na kutoa pasi za mwisho 100 - huku nusu yake zikienda kwa Messi - wakati walipotengeneza safu imara ya ushambuliaji na raia huyo wa Argentina na Neymar.

Ingawa wengi wanaweza kuona usajili huu ni mgumu kwa Suarez kurudi Barcelona, lakini anaweza kuwa na manufaa zaidi kwa kuhakikisha wanaungana na Messi.

**#4. Eric Garcia**

Nyota wa zamani wa akademi ya La Masia, Eric Garcia alikuwa mmoja wa wachezaji waliokuwa wanawaniwa na Barcelona kipindi cha majira ya joto kilichopita, lakini uhamisho huo haukufanikiwa - wakati bosi wa Manchester City, Pep Guardiola alipomwona kinda huyo kama mchezaji anayeweza kukaa hapo kwa kipindi kirefu zaidi.

Barcelona inahitaji kuimarisha safu yake ya ulinzi wakati Gerard Pique umri ukizidi kumtupa mkono, na kukosa nguvu na kasi yake kama mwanzo.

Garcia anaweza kuripotiwa kutua Barcelona wakati wa dirisha dogo la Januari. Kama hiyo itatokea, utakuwa usajili muhimu zaidi kwa wakati muafaka - na kuwezesha kuirudisha Barcelona kwenye nafasi yake ya kuleta ushindani na kutwaa mataji.

**#3. Georginio Wijnaldum**

Georginio Wijnaldum, ambaye amekuwa nguzo kubwa kwa Liverpool tangu kutua kwake pale Anfield miaka michache iliyopita, amekuwa akiwaniwa kwa muda mrefu na Barcelona.

Kiwango cha raia huyo wa Uholanzi kimekuwa kikimfanya kuwaniwa na timu nyingi, huku akiwa na ushirikiano mzuri na wachezaji wenzake kama Virgil Van Dijk, Mohamed Salah na Sadio Mane - ukiwataja kwa uchache. Aidha, Wijnaldum ni mmoja wa wachezaji muhimu sana kwa kikosi cha Jurgen Klopp.

Ukichukulia mchango wake kiungo huyo mwenye umri wa miaka 30, bila shaka yoyote ana nafasi kubwa zaidi ya kung'ara popote atakapokwenda.

Wijnaldum mwenyewe pia ameripotiwa kutaka kuungana na Messi pamoja na wachezaji wengine pale. Kama Barcelona wataweza kupata huduma yake, utakuwa usajili bora zaidi kwao.

**#2. Lautaro Martinez**

Lautaro Martinez, ambaye alikuwa na msimu wa kuvutia wa 2019-20 akiwa na Inter Milan, amekuwa akiwaniwa na Barcelona kwa muda mrefu.

Ingawa usajili wake haukufanikiwa kipindi cha majira ya joto kilichopita, Messi amekuwa akimzungumza mara kwa mara kuhusu raia mwenzake huyo wa Argentina. Nahodha huyo wa Barcelona hivi karibuni alizungumza kuhusu Martinez na kusema:

"Nafikiri tayari nimeshamtaja, kwamba Lautaro ni straika wa aina yake, na nafikiri yeye ni mshambuliaji aliyekamilika zaidi. Yuko imara, anafunga mabao, anajua namna ya kulinda mpira... lakini tutaona nini kitatokea kama nitakuwa naye au la."

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, anaweza kuwa patina mzuri zaidi wa Messi pale Barcelona. Lautaro mwenyewe tayari ameshaonyesha nia ya kutaka kucheza na Messi kama wanavyokuwa kwenye kikosi cha timu ya taifa.

Kutua kwa Martinez pale Camp Nou kunaweza kuongeza hamasa zaidi kwa 'Blaugrana' na kumfanya Messi kuendelea kubaki hapo Barcelona.

**#1. Neymar**

Neymar, alikuwa mmoja wa washambuiaji waliounda safu ya ushambuliaji ya Barcelona maarufu kama MSN (Mesi, Suares na Neymar), na kwa muda mrefu amekuwa akihusishwa na mpango wa kurudi tena pale Catalunya ambako aliondoka miaka mitatu iliyopita.

Raia huyo wa Brazil amekuwa na mahusiano mazuri zaidi na Messi ndani ya uwanja na nje ya uwanja, ambapo wawili hao walikuwa na upatina mzuri zaidi wa kufunga mabao.

Neymar kipindi cha majira ya joto kilichopita alihusishwa sana na mpango wa kurudi pale Barcelona, lakini uhamisho huo haukufanikiwa, ambapo miamba hao wa Catalunya hawakuwasilisha ofa yao mezani kwa PSG ili kumchukua mshambuliaji huyo.

Mbrazil huyo alifurahia mafanikio makubwa tangu kujiunga na PSG, akiifikisha klabu hiyo kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Hivi karibuni, Neymar alifunga mabao matatu 'hat-trick' dhidi ya Istanbul Basaksehir na kuisaidia timu yake kufuzu hatua ya mtoano ya timu 16-bora.

Katika mahojiano yake ya hivi karibuni, Neymar kwa mshangao wa wengi alizungumzia kuwa hana mpango wa kuondoka PSG. Hata hivyo, hilo linaweza kubadilika kama Barcelona wakiamua kumshawishi tena nyota huyo kurudi kwenye kikosi chao mwishoni mwa msimu huu.

Inaonekana wazi kabisa kwamba, Neymar hana uwezo wa kusema hapana kama akitakiwa kwenda kujiunga na Messi.

Ni wazi kabisa kwamba, kama Barcelona watamhitaji Neymar itakuwa kazi rahisi zaidi kumrudisha na kuungana na Messi pale Catalunya.

## Nukuu

"Hakutakuwa na mjadala kuhusu nani mwanasoka bora aliyewahi kushuhudiwa duniani - mimi au Pele. Kila mtu angesema mimi," **Diego Maradona enzi za uhai wake.**



"Tutakaa chini na [Lionel] Messi na kumwomba apunguziwe mshahara wake, kwa sasa namna mambo yalivyo ni jambo gumu kuendelea na mshahara uleule, tutamwomba kujitolea. Kama hakutakuwa na makubaliano, hivyo Messi ataondoka," **Mgombea Urais wa Klabu ya Barcelona, Emili Rousaud.**



"Kuna fedha nyingi kwenye soka kwa sasa, lakini kama hakuna njaa mchezaji kamwe hatafanikiwa. Unatakiwa kuangalia mchezaji ambaye ana njaa na nafikiri (Kylian) Mbappe ana kitu kama hicho na anahitajika kuichezea Real Madrid. Mimi si mwakilishi wake ila Mbappe, ana ubora na anafaa kuwachezea mabingwa wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Real Madrid," **straika wa zamani wa 'Los Blancos' hao, Davor Suker.**



Nipashe Spotika



# NTIBAZONKIZA NA 11 WALIOANZA KUFUNGUA AKAUNTI ZA MABAO

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji wa Yanga, Saido Ntibazonkiza, ameanza kuuwasha moto kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kuisaidia kwa kiasi kikubwa timu yake kupata ushindi wa mabao 3-1 kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha juzi, Jumamosi dhidi ya Dodoma Jiji FC.

Mchezaji huyo aliyesajiliwa kipindi hiki cha dirisha dogo akiwa mchezaji huru, aliingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Michael Sarpong, wakati huo ngoma ilikuwa ngumu, kwani timu zote zilikuwa sare ya bao 1-1.

Dakika ya 69, alifungua akaunti yake ya mabao Yanga kwenye mechi za Ligi Kuu Bara baada ya kutupia bao la pili kwa faulo ya staili ya mwezi mwandamo, ikagonga nguzo na mpira kutinga wavuni, akiipatia timu yake bao la pili.

Kama vile haitoshi, alipiga faulo iliyopita katikati ya wachezaji wa timu zote na kipa wa Dodoma Jiji, Aron Kalambo, lakini Bakari Mwamnyeto aliuwahi na kuutumbukiza wavuni.

Yanga iliingia mkataba na kiungo huyo, baada ya mechi ya kirafiki iliyokuwa kwenye Kalenda ya FIFA kati ya Taifa Stars na Burundi katikati ya Oktoba, mwaka huu na klabu hiyo ilikuwa inasubiria kufunguliwa kwa dirisha dogo Desemba 16, ili kukamilisha usajili wake Shirikisho la Soka nchini, TFF.

"Nitatumia uzoefu wangu wote kwenye klabu yangu, nikishirikiana na wenzangu ambao nimewakuta, basi tutafanya vizuri zaidi. Sioni ugumu wowote kwa sababu mimi ni mzoefu, najua ligi ni ngumu, lakini tutapambana," alisema Ntibazonkiza ambaye ameweka rekodi ya kuwa mmoja wa wachezaji kutoka nje ya nchi ambao hawakusubiri kuzoea ligi na badala yake walifunga mabao kwenye mechi za kwanza tu baada ya kusajiliwa.

Hawa ni baadhi ya wachezaji ambao walifunga mabao kwenye mechi za kwanza tu baada ya kusajiliwa...




Ntibazonkiza

**#1. Imeh Izuchukwu - Simba (2008/09)**

Ni mchezaji kutoka Nigeria ambaye alifunga bao kwenye mechi ya kwanza tu baada ya kusajiliwa na Simba, akiisaidia timu hiyo kushinda mabao 4-1 dhidi ya Villa Squad kwenye Ligi Kuu ya msimu wa 2008/09.

**#2. Benard Mwalala - Yanga (2008/09)**

Benard Mwalala, straika huyu kutoka nchini Kenya, alisajiliwa na Yanga msimu wa 2008/09 na mechi yake ya kwanza kucheza alipangwa dhidi ya Tanzania Prisons akifunga bao moja, Yanga ikishinda mabao 4-0.

**#3. Boniface Ambani - Yanga (2008/09)**

Pia ni straika Mkenya ambaye alijiunga na Yanga msimu wa 2008/09, na mechi yake ya kwanza tu kucheza alifunga mabao mawili kwenye mchezo ambao timu yake ilishinda mabao 4-0 dhidi ya Tanzania Prisons.

**#4. Emmanuel Okwi - Simba (2009/10)**

Ulikuwa ndiyo msimu wake wa kwanza kwa Emmanuel Okwi, mchezaji maarufu kabisa nchini Tanzania kuichezea Simba. Mechi yake ya kwanza, Simba ilicheza dhidi ya Toto Africans na alifunga bao, akiisaidia timu yake kushinda mabao 3-1.

**#5. Patrick Mafisango - Simba (2011/12)**

Alikuwa kiungo mkabaji wa Simba mwenye uwezo pia wa kushambulia na kufunga mabao. Alifariki hapa mwaka 2012 kwa ajili ya gari.

Mkongomani huyo mwenye uraia wa Rwanda naye pia anaingia kwenye orodha ya wachezaji kutoka nje waliosajiliwa na kufunga mechi zao za kwanza walizocheza. Alifanya hivyo msimu wa 2011/12, alipofunga bao kwenye mechi dhidi ya JKT Oljoro, Simba ikishinda mabao 2-0.

**#6. Didier Kavumbagu - Azam (2014/15)**

Mrundi huyo yeye ni mchezaji kutoka nje ya nchi, lakini alikuwa amejiunga na Azam akitokea Yanga. Mechi yake ya kwanza akiwa na Azam FC alifunga bao, wakati wakiichapa Polisi Morogoro mabao 2-1 msimu wa 2014/15.

**#7. Donald Ngoma - Yanga (2015/16)**

Mzimbabwe huyo aliingia kwenye orodha hiyo msimu wa 2015/16 alipofunga bao katika mechi yake ya kwanza, Yanga ikicheza dhidi ya Coastal Union, ikishinda mabao 2-0.

**#8. Laudit Mavugo - Simba (2016/17)**

Msimu wa 2016/17, Mrundi Laudit Mavugo, alifunga bao kwenye mechi yake ya kwanza tu alipojiunga na Simba ambayo ilicheza dhidi ya Ndanda na kushinda mabao 3-1.

**#9. Meddie Kagere - Simba (2018/19)**

Mnyarwanda Meddie Kagere naye aliingia kwenye orodha ya wachezaji walioanza ligi na kupachika mabao alipofunga bao pekee, Simba ikiifunga Tanzania Prisons 1-0 msimu wa 2018/19.


**#10. Heritier Makambo - Yanga (2018/19)**

Straika Mkongomani Heritier Makambo ameacha rekodi yake safi kwenye soka la Tanzania alipofunga bao dhidi ya Mtibwa Sugar msimu wa 2018/19, akiwa ndiyo kwanza amejinga na Yanga, ikishinda mabao 2-1.

**11. Michael Sarpong - Yanga (2020/21)**

Huyu ni straika raia wa Ghana, amefunga bao kwenye mechi ya kwanza akicheza kwa mara ya kwanza baada ya kusajiliwa na Yanga, wakati wakitoka sare ya 1-1 dhidi ya Tanzania Prisons.

**JE, WAJUA?**



POINTI 14 katika mechi 14, ilizozivuna Arsenal hadi sasa kwenye Ligi Kuu England msimu huu, ndio rekodi mbovu zaidi kwa klabu hiyo katika hatua kama hii ya msimu tangu msimu wa 1974-75, ilipovuna pointi 12.



# Waziri Jafo amtaka mkandarasi kukamilisha ujenzi kwa wakati

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, amemwagiza mkandarasi wa kampuni ya Chico, inayojenga barabara za urefu wa kilomita 52 kwa kiwango cha lami katika mji wa kiserikali, kukamilisha ndani ya muda.

Jafo aliyasema hayo juzi wakati alipofanya ziara ya kushtukiza kukagua ujenzi wa barabara hizo katika mji wa kiserikali Mtumba, kutokana na kasi ndogo ya ujenzi.

Alisema, ujenzi wa barabara hizo unatakiwa kukamilika kwa muda uliopangwa bila kuwapo kwa kisingizo.

"Niwapongeze tu leo ule mkwara wangu ulisaidia nimekuta kuna mabadiliko makubwa sana na kasi yenu ni ya kuridhisha hivyo basi nataka mradi huu ukamilike katika muda uliopangwa na siyo vinginevyo," alisema Jafo.

Pia, alimtaka mkandarasi huyo kuacha kutumia kisingizio cha kuadimika kwa saruji nchini ili kuchelewesha mradi huo.

"Kama hakuna saruji fanyeni kazi nyingine ambazo hazihitaji saruji, kama uchimbaji wa mitaro, lakini isiwe kama hakuna saruji basi na nyinyi mnakaa bila kufanya kitu chochote hamtakamilisha leo kwa mwenendo huu," alieleza Jafo.

Vile vile, Jafo alimwagiza mkandarasi huyo kuhakikisha ujenzi wa barabara hizo unafanyika usiku na mchana ili kukamilika ndani ya muda.

"Pamoja na kujenga usiku na mchana, lakini tunahitaji lami hii iwe kwenye viwango vya ubora siyo baada ya mwaka mmoja unakuja hapa unakuta mashimo kila eneo," alisisitiza Jafo.

Alimtaka mkandarasi huyo kuhakikisha kila siku ubora wa lami unapimwa ili kuondokana na dosari zinazoweza kujitokeza.

"Lazima mzingatie 'quality control' mpime lami hii kwenye maabara kila siku muache kufanya kazi kwa mazoea ndiyo maana hata katika viwanda vya soda wanapima kila siku vinginevyo soda kila siku zingekuwa na ladha tofauti," alisema Jafo.



Wafanyakazi wa Shirika la Majisafi na Majitaka DAWASCO, wakinyonya majitaka katika barabara ya Lumumba jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# TAKUKURU yaokoa mil. 45/- mradi wa maji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), mkoani Dodoma imeokoa Sh. milioni 45.7 alizolipwa mkandarasi wa kampuni ya Leostart Engineering ya jijini Dar es Salaam kinyume na utaratibu wa utekelezaji wa mradi wa maji wa kijiji cha Mlongila, wilayani Chemba, mkoani hapa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa, Mkuu wa Taasisi hiyo, Sosthenes Kibwengo, alisema fedha hizo ni sehemu ya alizolipwa mkandarasi huyo.

"Mtakumbuka siku za nyuma tuliwahi kuwataarifu kuhusu ufuatiliaji wetu wa mradi huo na ukaguzi maalum uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ulionyesha kuwa mkandarasi wa mradi huo wenye thamani ya Sh. milioni 579.323 ulioanza 2013 na kukamilika mwaka 2014, alilipwa fedha zaidi ya kazi zilizofanyika na hivyo kutakiwa kuzirejesha," alisema Kibwengo.

Alisema pia taasisi hiyo imefanikiwa kuwarejeshea zaidi ya Sh. milioni 18 zikiwamo Sh. milioni 9.7 za mfanyabiashara Dismas Kweka, mkazi wa Nkuhungu mkoani hapa na Sh. milioni 8.6 za Grace Matona, muuguzi mstaafu na mkazi wa jijini hapa.

Akitoa ufafanuzi, Kibwengo alisema Kweka aliuziwa kiwanja namba 18 kitalu B, kilichopo Mbwanga, jijini hapa kinyume na utaratibu na kuwa kiwanja hicho kilitolewa na mwananchi mmoja kama sadaka kwa Jumuiya ya Uamsho wa Wakristo Tanzania (UWATA). Alisema, fedha hizo zimerejeshwa kutoka kwa Richard Mwambeje ambaye alikuwa Katibu wa UWATA, alipokea Sh. milioni 19, baada ya kutengeneza mkataba wa kughushi na hivyo kutakiwa kurejesha fedha hizo.

"Mwambeje bado anatakiwa kurejesha fedha zilizosalia huku hatua nyingine za kiuchunguzi zikiendelea," alisema

Kuhusu fedha za muuguzi mstaafu, alisema ufuatiliaji wa TAKUKURU, umeonyesha kuwa mstaafu huyo aliipatia kampuni ya JW Micro Credit ya jijini hapa toka mwaka 2016 Sh. milioni 20, kwa ahadi ya kulipwa fedha hizo na faida, lakini hakulipwa faida wala fedha zake.

Katika hatua nyingine, Kibwengo alisema TAKUKURU kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Dodoma, imewasaidia wananchi watano kupata viwanja vyao ambavyo walidhulumiwa au kupatiwa eneo ambalo tayari lilikuwa na mmiliki mwingine. Aliwataka wananchi wanaohitaji viwanja kujiridhisha katika maeneo wanayohitaji kabla ya kulipa fedha.

"Hivi sasa Dodoma kuna matapeli wengi hasa katika eneo la viwanja, msikubali kulipa pesa yoyote kabla ya kwenda mamlaka husika kujiridhisha kuhusu umiliki wa eneo," alisema Kibwengo. "Tumemrejeshea mwananchi mmoja Sh. milioni 1.060 alizotapeliwa Job Makasi, mkazi wa Ipagala jijini Dodoma ambaye alimwahidi kumuuzia kiwanja chenye ukubwa wa mita za mraba 1,250 kilichopo eneo la Mlimwa 'C' kwa Sh. milioni 13."

"Hata hivyo, dalali huyo alikata mawasiliano tangu Agosti mwaka huu, baada ya kupokea malipo ya awali hadi tulipomtia nguvuni," alisema Kibwengo.

# TALIRI yapandikiza ng'ombe kupata mbegu bora

**Na Renatha Msungu,** MPWAPWA

TAASISI ya Utafiti wa Mifugo nchini (TALIRI), Kituo cha Mpwapwa imepandikiza mimba changa (viini tete) 34 kwa ng'ombe jike, kama majaribio ya awali ya kituo hicho, yanayolenga kuleta matokeo chanya kwa wafugaji.

Majaribio hayo yamefanyika baada ya TALIRI Mpwapwa kununua vifaa vyenye thamani ya Sh. milioni 400 vilivyotolewa na serikali kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH).

Mtafiti Kabuni Thomas, alisema hayo wakati akieleza hatua za awali za mradi wa uzalishaji mbegu bora za madume ya ng'ombe ambazo zitatumika kupanda kwa majike ili kupata ndama walio bora.

Thomas alisema utafiti wa awali unalenga kuleta mabadiliko kwa wafugaji, kwa sababu unakwenda kuzalisha ndama wenye ubora kwa wakati mmoja ambao watatoa faida kwa wafugaji watakapoanza kutoa maziwa.

"Teknolojia hii ni nzuri sana kama itatumiwa na wafugaji baada ya matokeo ya majaribio kutoka, wafugaji watanufaika ikiwamo kuinuka kiuchumi kutokana na kuwa na mifugo bora yenye uhakika wa kutoa maziwa kwa wingi," alisema Thomas.

Hata hivyo, alisema pamoja na kusubiri matokeo ya utafiti huo wanaiomba COSTECH kuendelea kuwapa sapoti ya fedha za mafunzo ya kuwajengea uwezo wataalamu wa uzalishaji mbegu za viini tete ambao watasambazwa katika vituo mbalimbali ili kuendesha programu hiyo ya TALIRI Mpwapwa.

"Kuendesha mafunzo kuongeza uwezo kwa watalaam kunahitaji fedha na hiyo ni changamoto kwetu tunaomba COSTECH wasichoke kutufadhili ili tuendelee kuongeza wataalamu wa kuzalisha viini tete," alisema Thomas.

Akielezea umuhimu wa wafugaji kutumia teknolojia ya uzalishaji mbegu bora za madume alisema itawapa faida kubwa ya uzalishaji maziwa, pia watakuwa na uhakika na kiwango cha maziwa kinachokamuliwa kwa siku, tofauti na anayetumia teknolojia ya asili.

Naye msimamizi wa Idara ya utafiti wa ng'ombe, Deogratius Masao, alisema teknolojia hii ikiwafikia walengwa muhimu itasaidia kuboresha mifugo yote ya asili kuibadilisha kuwa bora kutokana na kutumia mbegu bora za madume.

Alisema teknolojia hiyo ikipelekwa kwa jamii ya wafugaji itachangia kwa kiasi kikubwa kuwabadilisha wafugaji hao kuinuka kiuchumi.

Alisema kuna halmashauri nyingine tayari zimeanza kuonyesha matokeo chanya katika baadhi ya vijiji ambavyo walipewa idadi ya ng'ombe dume ambao bora.







Katibu Tawala Mkoa wa Mbeya, Mariam Mtunguja, akizungumza na wadau wa elimu wakiwamo wakurugenzi, maofisa elimu, waratibu na wenyeviti wa wilaya, mikakati ya kuongeza ufaulu matokeo ya darasa la saba, ambapo kwa mwaka 2020 mkoa umeshika nafasi ya 13 kati ya mikoa 26, hayo yaliyojili juzi, wakati wa kikao cha uchaguzi wa wanafunzi wanaotarajiwa kuanza kidato cha kwanza mapema Januari 2021. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Madarasa yakosesha 5,500 kidato cha kwanza

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WANAFUNZI 5,549 ambao ni miongoni mwa waliofaulu mitihani ya darasa la saba mkoani Mbeya, wamezuiliwa kuanza masomo ya kidato cha kwanza kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa.

Katibu Tawala Msaidizi Idara ya Elimu mkoani Mbeya, George Mbijima, ameyasema hayo wakati wa kikao cha uchaguzi wa wanafunzi waliofaulu mtihani wa darasa la saba mwaka huu kwa ajili ya kuanza kidato cha kwanza.

Mbijima alisema jumla ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka 2021 walikuwa 36,584 kati yao wavulana ni 17,224 na wasichana 19,360 na kati yao wanafunzi 31,035 wakiwamo wavulana 14,825 na wasichana 16,210 sawa na asilimia 84.8 waliochaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari.

Alifafanua kuwa asilimia 15 ya waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza ambao ni 5,549 wakiwamo wavulana 2,392 na wasichana 3,157 wamezuiliwa kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa. Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Mariam Mtunguja, alisema matokeo ya mtihani wa darasa la saba mwaka huu mkoani Mbeya hayaridhishi kutokana na mkoa huo kushika nafasi ya 13 kitaifa kati ya mikoa 26 Tanzania Bara.

Mtunguja alisema katika matokeo ya mwaka 2019 Mkoa wa Mbeya ulishika nafasi ya tano, mwaka 2018 ikishika nafasi ya 13, hali inayohitaji mikakati ya namna mkoa huo kuongeza ufaulu kwa kuwashirikisha wadau.

"Hali ya ufaulu mkoani Mbeya sio ya kuridhisha, tunahitaji mikakati ya kuongeza ufaulu nawaomba wakuu wa wilaya andaeni utaratibu wa kufanya vikao vinavyojikita katika kuhamasisha chakula shuleni," alisema Mtunguja.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Julius Chalya, amesema matokeo mabaya ya mtihani wa darasa la saba mkoani Mbeya yamesababishwa na mgomo baridi unaofanywa na baadhi ya walimu, huku Meya wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Duru Issa, akisema halmashauri yake inatarajia kukamilisha ujenzi wa vyumba 38 vya madarasa kabla ya Januari 30 mwaka 2021

# Taasisi yaonya uuzaji wa mbegu feki

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

TAASISI ya Udhibiti wa Mbegu (TOSCI), imetahadharisha kampuni zinazouza na kusambazaji mbegu kuacha kuwauzia wakulima mbegu feki kwa maelezo kuwa vitendo hivyo vinawaingiza wananchi hasara.

Mkaguzi wa mbegu wa TOSCI kutoka jijini Dodoma, Dk. Mngotosha Ngomuo, alitoa tahadhari hiyo juzi jijini Mbeya maofisa wa taasisi hiyo kutoka makao makuu na wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini walipofanya ukaguzi wa kawaida wa mbegu kwenye maduka yanayouza pembejeo.

Alisema mfanyabiashara atakayekamatwa anasambaza mbegu hizo atachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwamo kufikishwa mahakamani kwa maelezo kuwa vitendo hivyo vinafifisha juhudi za serikali kuinua kilimo.

Alizitaja mbegu ambazo zinatafsiriwa ni feki ni ambazo hazijakaguliwa na mamlaka hiyo na kuwekwa nembo, zilizopitwa na muda wake pamoja na zinaingia nchini kupitia njia za panya kutoka mataifa mengine.

"Kuna mbegu imeingia nchini kinyemela ikitokea nchi jirani ya Zambia, mbegu hiyo inasemekana inapatikana Mkoa wa Songwe hasa Wilaya ya Mbozi, nawaomba wananchi kuwa makini kwa kuzichunguza mbegu hizo kabla ya kwenda kupanda ili kujiridhisha," alisema Dk. Ngomuo. Alisema kwenye ukaguzi huo walibaini kuwa mbegu nyingi zinazouzwa kwenye maduka zimepitwa na wakati, hivyo wakazion-doa ili wafanyabiashara hao wasiendelee kuzisambaza.

Kwa upande wake mkaguzi wa mbegu kutoka Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mary Kilawe, aliwataka wadau kushiriki kuzuia usambazaji wa mbegu hizo kwa akiwataka kutoiachia TOSCI peke yake.

Alisema usambazaji wa mbegu feki una madhara makubwa kwa wakulima ikiwamo kuwasababishia wakulima hasara ya kutovuna kabisa mazao kama ambavyo wanakuwa wamekusudia. Aliwataka wauzaji wa mbegu hizo kuwa wazalendo kwa kuhakikisha wanaepuka kusambaza mbegu hizo, huku akisema wao ni wasimamizi wa sheria na hawapendi kuwachukulia hatawafanyabiashara na ndiyo maana wanatoa elimu.

"Tunajitahidi kutoa elimu ili wananchi hawa wasivunje sheria, sasa tukimkuta mtu ambaye tuna uhakika ana elimu, lakini anauza mbegu feki tafsiri yake inakuwa kwamba anafanya maksudi hivyo lazima tumchukulie hatua hali," alisema Kilawe.

Baadhi ya wafanyabiashara wa mbegu jijini Mbeya waliishukuru taasisi hiyo kwa kufanya ukaguzi huo, wakisema kuwa unasaidia kuwakumbusha baadhi ya kanuni na taratibu za uuzaji wa mbegu.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Yusta Mraki, alisema baadhi ya wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu ndio wanaoichafua shughuli hiyo kwa kuwafanya hata waaminifu waonekane hawafai.

Aliwaomba maofisa hao kuendelea kuwatembelea mara kwa mara hasa kipindi hiki cha kuelekea msimu wa kilimo ili kutoa elimu zaidi na kuzuia uuzwaji wa mbegu ambazo hazikidhi vigezo.

Baadhi ya wafanyabiashara nchini wamekuwa wakikosa uaminifu na wamekuwa wakiwauzia wakulima mbegu zisizokidhi viwango, ambapo mwaka jana baadhi wafanyabiashara walikamatwa jijini Mbeya wakitengeneza mbegu feki na kughushi nembo ya TOSCI.

# Walimu Kyela wataka ujenzi madarasa sita

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

WALIMU wa Shule ya Msingi Mwenge iliyoko Halmashauri ya Kyela, wameendelea kuikumbusha serikali kujenga vyumba vitano vya madarasa kwa ajili ya kuwasaidia watoto wenye mahitaji maalum.

Akizungumza katika mahojiano maalum na Nipashe, mwalimu wa kitengo cha kuwahudumia watoto wenye mahitaji maalum shuleni hapo, Benjamini Mwansombelo, anasema watoto wenye mahitaji maalum ambao wanafikia hatua nzuri ya uelewa darasani wanalazimika kurudi nyuma kwa sababu ya uhaba wa vyumba vya madarasa.

Mwalimu Mwansombelo alisema shule hiyo ambayo ni miongoni mwa zilizochagulia kuwafundisha watoto wenye mahitaji maalum, ina jumla ya watoto 41 ambao hulazimika kufundishwa kwenye darasa moja.

"Tatizo kubwa lililopo hapa shuleni kwetu ni uhaba wa vyumba vya madarasa na vifaa kwa ajili ya kuwafundisha watoto wenye mahitaji maalum, hali inayotulazimu hata wanafunzi wanaofanya vizuri kutoendelea mbele… tumejaribu kulitenganisha hilo darasa moja kwa kutumia mbao, lakini bado kuna mwingiliano wa kelele na shughuli nyingine zinazofanywa na hao watoto," alisema Mwalimu Mwansombelo.

Aliongeza kuwa jumla ya watoto 41 wenye mahitaji maalum 15 wana matatizo ya akili, waliobakia ni viziwi, vipofu, walemavu wa viungo na usonji.

Alisema utaratibu wa elimu kwa watoto wenye mahitaji maalum una ruhusu wakifika darasa la tatu kuanza kujichanganya na wenzao kupitia mfumo wa elimu jumuishi na kama hawaelewi wanawapima kwa majaribio wakibaini hawajaelewa wanakaa nao kuwaelekeza.

Alisema utaratibu huo umesaidia kujenga urafiki nao wako huru kueleza shida zao na kuelewa kwa urahisi. Alisema kabla ya kuanzishwa kitengo cha kuwahudumia watoto wenye mahitaji maalum shule ilikuwa ikiwahudumia watoto wa kawaida, hivyo miundombinu iliyopo haikidhi mahitaji ya wenye ulemavu.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Jona Kanyeka, alisema kitengo maalum kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalum shuleni hapo kilianza mwaka 2012. Alisema kuna uhitaji mkubwa wa miundombinu kwa watoto wenye ulemavu hususani viwanja vya michezo, uzio, vifaa vya kufundishia na kujifunzia pamoja na madarasa.

Aliongeza kuwa hadi sasa kuna jumla ya walimu watatu akiwamo mmoja wa kujitolea ambao wanawafundisha watoto hao hitaji likiwa ni walimu sita.



# Vijana waonyeshwa fursa kujiajiri usafi mazingira

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Tawala wa Wilaya ya Magharibi 'B' Unguja, Makame Machano Haji, amesema vijana wa Zanzibar wanafursa kubwa za kujiajiri na kuondokana na hali ya utegemezi.

Alisema Zanzibar kuna tatizo kubwa la kimazingira na kijamii na kulipongeza shirika la kusaidia jamii wanaoishi katika mazingira holela kutatua changamoto za kimazingira (CCI), kwa kuwekeza miradi yao Zanzibar kwa lengo la kuwakomboa vijana na wanawake kupitia fursa mbalimbali zilizowazunguka ikiwamo ya usafi wa mazingira.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua mkutano wa wadau wa mazingira ulioandaliwa na Taasisi ya CCI uliofanyika mjini Unguja.

Alisema Zanzibar ina utajiri mkubwa wa bahari ni namna ya kushughulikia ili wananchi wapate maendeleo.

Alisema Zanzibar ina tatizo kubwa la mazingira na kijamii na shirika hilo linafanyia kazi eneo hilo na kukuza mitaji ya vijana na wanawake ili kujikomboa kimaisha kwa kuwa vijana na wanawake wanaathirika zaidi katika eneo hilo.

Feso Domanic Makoba, Mhandisi wa Maji na Usafi wa Mazingira wa Shirika la CCI, alisema shirika hilo linatekeleza mradi wa kuondoa uchafu ikiwamo kinyesi cha binadamu na kukibadilisha kuwa gesi ya kupikia.

Alisema changamoto ya kimazingira ni kubwa ikiwamo vyoo kujaa na kwamba mradi huo una lengo la kuweka usafi wa mazingira katika maeneo mbalimbali ya mjini na vijijini.

Alisema mradi huo umeleta faida kubwa kwa sababu kinyesi kipo kingi na wamefanikiwa kujenga vyoo bora katika jamii na kinyesi hicho kukibadilisha kuwa gesi kwa ajili ya kupikia.

"Changamoto (tatizo) za kimazingira zilikuwa nyingi hasa wanaoishi katika makazi holela ikiwamo la vyoo kujaa mara kwa mara hivyo, faida moja wapo ni kuweka mazingira salama na suluhisho la nishati mbadala," alisema.

Naye Mwanakombo Mkanga, mwakilishi wa taasisi ya CCI, alisema taasisi hiyo imewezesha vijana kupata ajira kwa kujiajiri katika miradi mbalimbali baada ya kupewa elimu.



Mwenyekiti wa Baraza la Kiswahili, Dk. Mohamed Seif (kulia), akimkabidhi vitabu mbalimbali na maandiko tofauti ya Kiswahili yaliyoandikwa na Waswahili kutoka maeneo tofauti. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wataalamu lugha Kiswahili watakiwa kuilinda

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WATAALAMU wa lugha ya Kiswahili Zanzibar wametakiwa kuhakikisha kwamba lugha hiyo pamoja na lahaja zake zote inalindwa, inaendelezwa na kukuzwa ili izidi kuzungumzwa na kutumika katika mambo mengi zaidi kwenye ngazi ya kitaifa na kimataifa.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, aliyasema hayo juzi wakati akifungua kongamano la nne la Kiswahili la kimataifa, Kikwajuni mjini hapa.

Alisema lugha ya Kiswahili lazima iwe na misamiati ya kutosha katika nyanja ya kiufundi, teknolojia ya habari na mawasiliano, sanaa, sheria, michezo, dini na nyanja zote za kiuchumi kwa lengo la kuwa na nguvu kubwa itakayojitosheleza ili kuepuka kuwa fukara kwa kutegemea misamiati ya lugha nyingine.

Alisema kumekuwa na utamaduni wa kukivuruga Kiswahili bila aibu hasa kwa wanajamii wengi ambao hufuata mkumbo na kuleta athari isiyopendeza katika matamshi ya lugha yenyewe yenye lahaja za kupendeza katika uzungumzaji.

Hemed alisema wanahabari na wasomi ndio wanaotegemewa katika kuiendeleza lugha ya Kiswahili, na kwamba ni vyema kuwa makini katika matumizi yake hasa wakati wanapotoa taarifa mbalimbali kwa wana jamii.

"Mnahitaji mjue jinsi ya kuteua maneno na pale mnapokosa uhakika wa uteuzi wa maneno muafaka basi ulizeni kwa wanaojua. Eleweni kwamba nyinyi ndio mnaosikika kwa haraka zaidi na kuigwa na wanajamii," alisema Hemed.

Alisema amevutiwa na juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) kwa kushirikiana na taasisi tofauti za serikali na za kiraia katika kuandaa kongamano hilo kila mwaka linalowajumuisha wataalamu waliobobea katika lugha ya Kiswahili waliopo Zanzibar, ukanda wa Afrika Mashariki na nchi zingine za mabara ya Amerika na Asia.

Alisema umuhimu wa kongamano la Kiswahili la kimataifa unazidi kuonekana kila mwaka kutokana na mafanikio yanayopatikana ambayo yamesaidia kuwezesha kwa sasa lugha ya Kiswahili kuwa miongoni mwa lugha kubwa kimataifa.

Alisema zipo takwimu na baadhi ya vitabu vilivyoandikwa vikionyesha lugha hiyo imekuwa ya saba kati ya zinazozungumzwa na idadi ya mataifa mbalimbali kukiwa na idadi ya wanaozungumza na kukifahamu inayokisiwa kufikia watu milioni 160, na idadi inayoongezeka kwa haraka kadri ya miaka inavyosonga mbele.

Alisema tafsiri ya takwimu hizo ni kwamba juhudi hizo za pamoja za kukikuza na kukitangaza Kiswahili zinaendelea kutoa matunda mazuri hasa kwa vile tayari kimesharidhiwa kuwa lugha inayozungumzwa ndani ya mikutano ya viongozi wa Umoja wa Afrika (AU) na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC).

Naye Mwenyekiti wa Baraza la Kiswahili Zanzibar, Dk. Mohamed Seif Khatib, alisema moja kati ya kitu adhimu kwenye mjumuiko huo ni washiriki wa kongamano hilo kutengewa muda mahsusi wa kutembelea maeneo ya kihistoria.

Kwa upande wake Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita, alisema kuendelea kufanyika pamoja na ushiriki wa wadau wa Kiswahili ni moja ya heshima kubwa inayoipata Zanzibar.

Tabia alisema dhamira ya kongamano hilo inadhihirisha wazi kasi ya serikali katika kuendeleza nguvu zake kwenye uchumi ndani ya mwelekeo wa uchumi wa buluu ambao machapisho ya lugha ya Kiswahili katika bidhaa zinazoingia kwenye soko la utalii yataendelea kupata nafasi.

# Wakulima viungo kunufaika mradi wa Euro mil. 5

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAKULIMA 21,000 kutoka katika maeneo mbalimbali Unguja na Pemba wanatarajiwa kunufaika na mradi wa kukuza kilimo cha mboga, matunda na viungo (viungo Project), katika shehia zaidi ya 50, unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU), wenye gharama ya Euro milioni tano.

Meneja utafiti na ufuatiliaji wa mradi huo, Ally Mbarouk, alisema hayo wakati alipokuwa akizungumza na maofisa wa halmashauri, mjini hapa.

Alisema mradi huo wa miaka minne unaotekelezwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA-Zanzibar), Jumuiya ya Kuhifadhi Mazingira Pemba (CFP) pamoja na Taasisi inayojihusisha Maendeleo ya watu kutoka Dar es Salam (PDF), unalenga kuhamasisha zaidi kwenye kilimo kilichobora.

Alisema mradi huo utatekelezwa katika wilaya tisa za Zanzibar, tano kutoka kisiwa cha Unguja na nne kutoka kisiwani Pemba na maeneo yote yamezingatia ushauriano wa wataalamu wa wizara ya kilimo.

Alisema miongoni mwa malengo makuu ya mradi huo ni kuwaweka karibu wadau wote wanaohusika na uzalishaji wa mazao mbalimbali na kuongeza ubora wa uzalishaji kwa bidhaa za kilimo pamoja na kuongeza lishe na uhakika wa chakula kwa wakulima Zanzibar.

Alisema pia mradi huo utaongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa ikiwamo kuboresha masoko ya nje na ndani ya nchi na kubainika kwa miaka mingi bidhaa za Zanzibar zimeshindwa kufanya vizuri katika masoko ya nje ya nchi.

Akitaja baadhi ya mikakati waliyokusudia ni pamoja na kutoa elimu ya kilimo bora kisichotumia mbolea zenye madhara kwa walaji kutokana na watu wengi kwa sasa kukataa bidhaa zinazozalishwa kwa kutumia mbolea isiyokidhi vigezo.

Katika hatua nyingine, alisema kupitia washirika wao kwenye mradi huo, Taasisi ya Kimataifa inayojihusisha na Uhifadhi wa Misitu (CFI), yenye makazi yake nchini Canada, wamekusudia kukuza soko la bidhaa za Zanzibar katika mataifa mbalimbali ulimwenguni kwa lengo la kutoa fursa zaidi.

Aliwataka maofisa wa halmashauri na watakaohusika na mradi huo kutoa ushikiriano kuhakikisha utekelezaji huo unafanikiwa kwa kiwango kikubwa ili kuunga mkono juhudi za serikali kuwaletea maendeleo wananchi wake.

Alisema anaamini kuanza kwa mradi huo kutafungua fursa kubwa zaidi na kuinua uchumi kwa wananchi wengi kwa kuzingatia kasi ya maendeleo ya uongozi wa serikali.

Washiriki wa mafunzo hayo walisema mradi huo umekuja wakati mwafaka kwa wananchi wengi Zanzibar wanahitaji maendeleo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**
Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:
- **Kuboresha biashara**
- **Kulipa kodi ya nyumba**
- **Kumalizia tenda**
- **Kulipa matibabu n.k.**

Mawasiliano yetu:
**Dar es salaam - 0768 928 516.**
**Arusha - 0677 226 960.**

## NAFASI ZA SHULE


**Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.**

## TUNAHITAJI MAFUNDI

**TUNAHITAJI MAFUNDI WA PIKIPIKI WENYE UZOEFU, UMRI MIAKA 25-35.**
**TUMA MAOMBI KWA: linkallafrica@gmail.com**
**MWISHO WA KUTUMA MAOMBI NI: 17/12/2020.**

NIPASHE NI JIBU LAKO
NJOO UTANGAZE NASI
KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0782253676

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**BAHATI BONIPHACE KAZUZU** anatangaza kupotelewa na Hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE 188137** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam **tarehe 07/09/2019.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
**Control No. 9910819362788.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**LILIAN MUNDHARI** anatangaza kupotea kwa cheti chake cha kidato cha sita chenye index namba **S0417-0515** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MWAKALELI SEKONDARI mwaka 2012. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/869182/2020.**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**

Katikamahakamayamwanzo**DODOMAMJINI** Usimamizi wa mirathi **No.182/2020** Ombi la **ATHUMANI SAIDI** kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu **ZENA H. KUNGA** Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo **tarehe 24/12/2020** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo. Wosia ya Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. **Tarehe 17/12/2020.**

## KUPOTEA KWA PASSPORT

**BAHATI BONIPHACE KAZUZU** anatangaza kupotelewa na Hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE 188137** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam **tarehe 07/09/2019.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. **Control No. 9910819362788.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**CHINA ROAD & BRIDGE CORPORATION(T)LTD** inatangaza kupotelewa na kadi za magari kama ifuatavyo,**REG No T 478 AAG** aina ya **MITSUBISHI , MODEL: FUSO,CHASSIS No. FV4155-A42101,ENG No 440541,** na kadi ya gari aina ya **REG No T 460 AAG, MITSUBISH, MODEL FUSO,CHASSIS FV 415J-A43606 CONTROL No. 9910819421807** KWA YEYOTE MWENYE TAARIFA APELEKE KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILCHO KARIBU NAYE.

## NOTISI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Sisi **Dabri Auction Mart Company Limited** kwa idhini tuliyopewa na **Benki ya Letshego** na mamlaka tulionayo kisheria tunatoa notisi ya siku 14 kuanzia siku ya tangazo hili kwa mdaiwa na mdhamini walipe deni lao lote kinyume na hapo tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara dhamana zao.

| S/N | JINA LA MKOPAJI | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | ENEO ILIPO DHAMANA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | ANGANILE MWAMBULUMA ANDREW | ANGANILE MWAMBULUMA ANDREW | NYUMBA YENYE HATI NA.34486 KIWANJA NA. 305 KITALU D | MBALIZI AREA-MBEYA | TAREHE 31/12/2020 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA.**
1. Mnunuzi atalazimika kulipia 25% ya bei iliyofikiwa kwenye mnada na salio la 75% litalipwa ndani ya siku 14 tangu siku ya mnada.
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipia salio ndani ya siku 14, atakua amepoteza haki yake ya malipo ya 25% na dhamana itauzwa tena.
3. Gharama zote kuhusu kubadilisha jina na umiliki wa dhamana zitakua juu ya mnunuzi.

**Kwa maelezo zaidi fika kwenye ofisi zetu zilizopo Mwananyamala au wasiliana nasi kwa namba za simu 0713401175 na 0657507050**

Uza,
Chenye Thamani Kubwa Kwa
Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa
Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

# Wapewa onyo la mwisho migogoro migodi midogo

**Na Happy Severine, SIMIYU**

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, ametoa onyo la mwisho kwa baadhi ya wafanyabiashara wa madini ambao wamekuwa chanzo cha migogoro kwenye migodi midogo nchini.

Biteko alitoa onyo hilo, mwishioni mwa wiki mbele ya wachimbaji wadogo wa mgodi wa Rubaga, ulioko mpakani mwa Wilaya ya Busega na Bariadi mkoani Simiyu.

Alisema migogoro kwenye migodi midogo imezidi na imekuwa kero ambapo ameeleza baadhi ya wafanyabiashara ndiyo wamekuwa chanzo cha migogoro hiyo.

"Tunayo majina ya baadhi ya wafanyabiashara ambao wamekuwa chanzo cha migogoro kwenye migodi hii midogo imezidi na imekuwa kero kila siku, tumechoka.

"Tunajua wanaanzisha hii migogoro ili waweze kutorosha madini, nawaambia siku zao zimefika... wamefanya huko na sasa wameanzisha huku Simiyu, serikali hatuwezi kuwavumilia," alisema Biteko.

Biteko alisema kuwa bado kwenye migodi midogo midogo, utoroshaji wa madini umekuwa mkubwa, hivyo amewataka viongozi wa mkoa na wilaya kusaidia katika kudhibiti wizi huo.

Alieleza kuwa wizara yake imeanza kuchunguza watu wote ambao wanafanya vitendo hivyo kutorosha madini, kwani majina yao wanayo na watachukuliwa hatua kali mmoja mmoja.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Ummy Mwalimu (kushoto), akishirikiana na Mkuu wa Mauzo wa Vodacom Tanzania PLC Kanda ya Kati, Grace Chambua (kulia), na wadau wengine kufunua pazia kuzindua rasmi bustani ya msitu wa miti ya kupandwa, katika eneo la Medeli, jijini Dodoma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwakyembe ataka vitabu kuwapigania yatima

**Na Thobias Mwanakatwe**

MWENYEKITI wa Baraza la Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), Dk. Harrison Mwakyembe, ametoa wito kwa watunzi wa vitabu kuandika vinavyopigania haki za yatima na maskini.

Alisema hayo jana, jijini Dar es Salaam, wakati wa uzinduzi wa kitabu cha Nguvu ya Ufalme wa Mungu kilichoandikwa na Mtume Annette Ashura Kawawa ambacho kimeandikwa kwa lugha tatu, Kiswahili, Kiingereza na Kifaransa.

Dk. Mwakyembe alisema kuwapigania yatima na maskini ni jambo jema sana, ili nao waweze kupata haki zao, na ndio maana hata katika Biblia Takatifu kuna maneno 406 ya maskini na umaskini.

"Katika Biblia kuna neno rushwa ambalo linapingwa sana kwa sababu rushwa ikishamiri inamuumiza maskini, Mungu hapendi rushwa kwa sababu inamuumiza maskini wake," alisema na kuongeza:

"Sisi sote hapa duniani ni watoto wa Mungu, hivyo hata kila tunapofanya jambo baya mfano rushwa Mungu anatuona, hivyo kila mtu achukue hatua kukabiliana rushwa."

Dk. Mwakyembe aliwapongeza viongozi wa dini kwa jitihada wanazofanya katika kusaidia yatima na watu wasiojiweza, na kwamba jamii inatakiwa kuiga mfano wa viongozi hao.

Kwa upande Mtume Annette wa Kanisa la Mercy Faith House of Player, alisema kitabu hicho kimebeba maono na nguvu ya Mungu na kuwaondolea watu mateso.

Alisema huduma anayoitoa inalenga zaidi kusaidia yatima, na kwamba eneo lilipojengwa kanisa ambalo lipo ndani ya nyumba yake iliyopo Mikocheni, palikuwa na bwawa la kuogelea, lakini aliamua kulifunika na kuanzisha ujenzi wa kanisa.

Annette aliamuru fedha zilizopatika kutokana na kuuzwa vitabu kwa walikwa wakati wa hafla hiyo zitapelekwa kwa yatima ili ziwasaidie kufurahia wakati wa sikukuu ya Krismasi.

# Wanaharakati watathmini faida masuala ya kijamii

**Na Yasmine Ptotace**

WANAHARAKATI wa semina za maendeleo ya jamii (GDSS), wamefanya tathmini ya mwaka mzima juu ya masuala ya kijamii, na kueleza faida walizozipata kupitia mafunzo hayo.

Mwajuma Hamis, mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, alisema ameweza kunufaika na mafunzo hayo na kufanikiwa kutoa msaada kwa jamii kupitia mafunzo hayo.

"Ni mwaka sasa toka Januari hadi Desemba mwaka huu, tumepatiwa mafunzo mbalimbali ikiwamo mambo ya mirathi na mafunzo hayo yamenisaidia...na mimi nimeweza kuyatoa kwa jamii na imeweza kujua masuala ya mirathi, ikiwamo na kupambana na matukio ya ukatili," alisema.

Mshiriki mwingine, Hamis Juma, alisema kuwa katika tathmini za mada mbalimbali zilizokuwa zikijadiliwa kwa kipindi cha mwaka mzima tangu Januari 2020 hadi Desemba 2020 zimesaidia kueleza wanajamii namna ambavyo wamepata mafunzo kupitia semina hizo zinazoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP).

Alisema semina hizo zimekuwa mkombozi kwao kutokana na kupatiwa mafunzo yaliyowapa uelewa.

Tumepatiwa mafunzo mbalimbali na yametusaidia kujua masuala ya wosia, mirathi, ushiriki wa wanawake katika mgawanyo wa majukumu, mlengo wa bajeti na masuala ya ukatili wa kijinsia," alisema.

Akizungumza kwenye semina hizo zinazoandaliwa na TGNP, Ofisa Programu Idara ya Habari na Mawasiliano, Jackson Malangalila, alisema wamefanya tathmini ya kile walichojifunza kwa mwaka mzima na kuwataka wanajamii kueleza kile ambacho wamekilewa kutoka katika semina hizo.

"Mwezi huu ni GDSS ya mwisho ambayo inaanza Januari hadi Desemba, hivyo washiriki wa semina hizo ambazo ufanyika kila Jumatano, wameweza kuelezea walichojifunza na jinsi walivyoweza kunufaika na mafunzo hayo," alisema.

Alisema washiriki mmoja mmoja kwa nyakati tofauti walisema wamenufaika na masuala mbalimbali ikiwamo elimu uwezeshwaji kiuchumi kwa makundi mbalimbali ya vijana na wanawake.

HABARI MICHEZO




# RONALDO

## AJIWEKEA REKODI YAKE SERIE A

**TURIN, Italia**

CRISTIANO Ronaldo alionyesha "namna gani anajali" kuhusu kufunga mabao wakati akiwa mchezaji wa kwanza kwenye Serie A tangu mwaka 1961 kufikisha mabao 33 ndani ya kalenda ya mwaka mmoja kwenye Ligi Kuu Italia.

Ronaldo alifunga mara mbili wakati Juve wakiibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Parma, huku mengine yakifungwa na Dejan Kulusevski na Alvaro Morata.

Mchezo huo ulikuja ikiwa ni siku tatu tangu Ronaldo akose penalti wakati Juve wakilazimishwa sare ya bao 1-1 na Atalanta.

Pirlo alionyeshwa kufurahishwa na rekodi hiyo ya Ronaldo ambaye kwa sasa ana umri wa miaka 35.

"Ronaldo alikuwa na hasira baada ya kukosa penalti, lakini tulikuwa na siku chache ya kufikiria kuhusu hilo na alionyesha namna gani anajali kufunga mabao," alisema Pirlo akinukuliwa na tovuti ya Juventus.

"Hatukuwa na furaha na matokeo ya Jumatano, lakini kiwango kilikuwa kizuri. Tulilazimika kuhakikisha tunapata pointi dhidi ya Atalanta na tulifanikiwa kufanya hivyo."

Omar Sivori ndiye alikuwa mchezaji wa mwisho kwenye Serie A kufunga mabao 33 kwa kipindi cha mwaka mmoja.

## ARTETA: NAJUA PRESHA INAYONIKABILI ARSENAL

**LONDON, England**

MIKEL Arteta anaelewa namna gani alivyo kwenye presha kubwa baada ya Arsenal kuendelea kuwa na matokeo mabaya kwenye Ligi Kuu England, wakati alipochezea kichapo cha mabao 2-1 kutoka Everton, Jumamosi.

Penalti ya Nicolas Pepe ilisawazisha bao la kujifunga la Rob Holding kwenye dimba la Goodison Park, lakini Yerry Mina akafunga na kuwapa ushindi huo Everton.

Arsenal imefikisha pointi 14 katika mechi 14 ambapo ni mwanzo mbaya zaidi katika historia yao kwenye ligi hiyo tangu msimu wa 1974-75.

Huku klabu yake ikiwa juu kwa pointi nne tu kutoka mstari wa kushuka daraja, Arteta amesema anaelewa presha inayomkabili.

"Kiukweli ni hali inayochanganya, lakini bado ina hamasa kubwa kutoka kile ninachokiona kutoka kwa wachezaji kujaribu na kuendelea kufanya kile wanachopaswa kufanya.

"Bila shaka, tunahitaji kuimarika," alisema kocha huyo wa Arsenal akiwaambia waandishi wa habari.

"Lakani yote kwa yote, tumekuwa hatuna bahati kabisa, tumeshindwa kabisa kupata pointi nyingi katika hatua hii."

Arteta aliongeza: "Nguvu na akili yangu kwa sasa nataka timu iondokane na hali hii, ili irudi

## LEWANDOWSKI, MULLER WATABIRI MAKUBWA KWA SANE BAYERN

**MUNICH, Ujerumani**

ROBERT Lewandowski na Thomas Muller wana matumaini Bayern Munich itamfanya kuwa bora zaidi Leroy Sane mwakani, baada ya winga huyo kutolewa kwenye mchezo dhidi ya Bayer Leverkusen.

Sane amekuwa na wakati mgumu tangu ajiunge na Bayern akitokea Manchester City kwa ada ya awali ya euro milioni 49 Julai, mwaka huu huku akiwa amefunga mabao matano tu kwenye Bundesliga.

Alianzia tena benchi kwenye mchezo wa Jumamosi pale kwenye dimba la BayArena, lakini alipewa nafasi kipindi cha pili akichukua nafasi ya Kingsley Coman.

Hata hivyo, alicheza kwa dakika 36 kabla ya kutolewa nje na nafasi yake kuchukuliwa na Jamal Musiala.

Sane alionekana mwenye hasira wakati akitoka uwanjani na kwenda benchi, lakini kocha Hansi Flick alibainisha kwamba, hakuna namna nyingine zaidi ya kufanya mabadiliko.

"Haikuwa adhabu," alisema wakati wa mkutano wake na waandishi wa habari.

"Nililazimika kufanya mabadiliko, na chaguo lilikuwa kati ya Thomas Muller, Serge Gnabry au Leroy."

Lakini Muller alionekana kumtetea Sane na kusema kwamba, hakupaswa kutolewa mapema hivyo.

"Hansi lazima awe na sababu," alisema Muller kuhusu Sane kutolewa uwanjani.

"Binafsi napenda sana kucheza na Leroy na nafikiri tulikuwa na wakati mzuri zaidi pamoja."

Naye Lewandowski ambaye alifunga mara mbili kwenye mchezo huo likiwamo la ushindi dakika ya 93, alisema Sane anapaswa kupewa muda zaidi.

"Anahitaji muda kuweza kuwa kwenye ubora wake," alisema Lewandowski akimzungumzia Sane.

## HABARI MICHEZO



# SHEARER

## ARSENAL KUSHUKA DARAJA

**LONDON, England**

ALAN Shearer "hana uhakika" kama Arsenal inaweza kubaki kwenye Ligi Kuu England mwishoni mwa msimu huu.

'Washikabunduki' hao wamekuwa na mwanzo wa msimu mbaya zaidi tangu msimu wa 1974-75 na sasa wapo nafasi ya 15 kwenye msimamo.

Wamepata pointi 14 katika mechi 14, wamefungwa nane kati ya hizo kwenye Ligi Kuu msimu huu.

Alipoulizwa kama wataweza kubaki kwenye Ligi Kuu, Shearer alijibu: "Sina uhakika na hilo. Kwa ari ya timu na baadhi ya wachezaji wake, sidhani."

Kipigo cha mabao 2-1 kutoka kwa Everton pale kwenye dimba la Goodison Park Jumamosi kilikifanya kikosi hicho cha kocha Mikel Arteta kuwa juu kwa pointi nne tu kutoka mstari wa kushuka daraja.

Washikabunduki hao hawajafunga bao la wazi katika mechi zake tano za ligi nyumbani na ugenini.

Nicolas Pepe, ambaye ni mchezaji aliyesajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi klabuni hapo ya pauni milioni 72, alifunga kwa penalti bao lake la pili kwenye Ligi Kuu msimu huu.

Shearer aliongeza: "Wachezaji hawana ubunifu, wachezaji hawajitumi na wacheza ilimradi tu.

"Mikel Arteta anaweza kuwa ndiye mtu mwenye hofu kubwa kwa sasa akijaribu kuokoa kibarua chake."

# STERLING AZUNGUMZIA USHINDI WA MAN CITY

**MANCHESTER, England**

RAHEEM Sterling amebainisha kwamba, Manchester City "walizungumza kwa kina" wao wenyewe kabla ya kwenda kushinda dhidi ya Southampton.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa England alifunga bao pekee pale kwenye dimba la St Mary's wakati City wakiibuka na ushindi wa bao 1-0 kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya England, Jumamosi.

Katika siku ambayo Liverpool ilifunga mabao saba dhidi ya Crystal Palace, ushindi huo mwembamba kwa City ulikuwa na hamasa kwao baada ya kutoka sare mbili mfululizo dhidi ya Manchester United na West Brom.

Na Sterling baada ya mchezo huo aliwaambia waandishi wa habari kwamba, walilazimika kuzungumza wao wenyewe ili kujipa hamasa na kuhakikisha wanaondoka na ushindi kwenye mchezo huo.

Alisema: "Kushinda mchezo na kufunga limekuwa jambo gumu kwa siku za hivi karibuni kwa upande wetu, lakini tulijua namna gani ni muhimu kushinda na kupata pointi zote tatu.

"Tulizungumza wenyewe na kujipa hamasa. Tulitakiwa kuhakikisha tunapambana ili kupata matokeo, sababu hii ni timu kubwa na tunatakiwa kupambana katika kila mchezo."




# DYBALA NI MUHIMU SANA JUVENTUS - PIRLO

**TURIN, Italia**

ANDREA Pirlo amesisitiza Paulo Dybala ni muhimu kwake licha ya uvumi kuendelea kuhusu majaliwa yake kwa straika huyo wa Juventus.

Dybala mwenye umri wa miaka 27, amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka kwa mabingwa hao wa Serie A, licha ya matarajio kwamba anaweza kuongeza muda wake wa kukaa pale Juve, ambapo mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2022.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina, ambaye amekuwa akihusishwa na Manchester United, alikosa mchezo wa Jumamosi wa ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Parma kutokana na kuumia nyama za paja.

Alipoulizwa kama Dybala alikuwa muhimu kwake, kocha huyo wa Juve, Pirlo aliwaambia waandishi wa habari: "Kiukweli kabisa. Mabingwa kama yeye mara zote ni watu muhimu kwa timu imara."

Pirlo ana matumaini Dybala atarudi haraka dimbani wakati kesho Jumanne Juventus watakaivaa Fiorentina.

"Nimefanya mazoezi na wachezaji wote. Dybala ni mmoja wao. Tabia yake ni nzuri," alisema.

"Bahati mbaya alipata majeraha na jana (juzi) alijaribu kulazimisha, lakini alihofia kuumia zaidi. Tunatumaini tutakuwa naye Jumanne."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# PELE AMSIFU MESSI KUFIKIA REKODI YAKE

●●●Hongera sana kwa kuifikia rekodi hiyo, habari yako ni kama yangu, kuipenda klabu moja kwa...

**SAO PAULO, Brazil**

PELE amempongeza Lionel Messi kwa kufikia rekodi yake ya kufunga mabao mengi zaidi kwa klabu na kusema anavutiwa sana na nyota huyo wa Barcelona.

Messi alifunga bao lake la 643 kwa Barca wakati wakitoka sare ya kufungana mabao 2-2 nyumbani na Valencia kwenye mchezo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Jumamosi.

Mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or aliifikia rekodi ya Pele ya kufunga mabao 643 katika mechi 656 kwa klabu yake ya Santos kati ya mwaka 1956 na 1974.

Pele, anachukuliwa na wengi kama ndiye mchezaji bora wa wakati wote wa soka duniani, alituma posti yake ya kumpongeza Messi kwenye ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Instagram.

"Wakati moyo wako unapokuwa unatiririka na mapenzi, ni ngumu kubadilisha njia yako," aliandika gwiji huyo wa Brazil.

"Kama wewe, najua namna gani unapenda kuvaa jezi ile ile kila siku. Kama wewe, najua hakuna sehemu bora kama ile inayohisi kama upo nyumbani.

"Hongera sana kwa kuifikia rekodi hiyo katika historia yako ya soka, Lionel. Lakini juu ya yote, hongeza kwa kipindi chako kizuri hapo Barcelona. Habari yako ni kama yangu, kuipenda klabu moja kwa muda mrefu, bahati mbaya kwa soka la kisasa ni nadra sana.

"Unanivutia sana,@leomessi."

Awali penalti yake kwenye mchezo huo iliokolewa na Jaume Domenech, lakini Messi alifikisha idadi hiyo ya mabao kwa kuunganisha kwa kichwa krosi iliyotoka kushoto na kufunga kiurahisi.

Bao hilo la kichwa kwa Messi lilikuwa la kwanza kwake kwa Barcelona katika mashindano yote tangu Machi mwaka 2017, huku akikosa penalti yake ya kwanza kwa klabu hiyo tangu Februari mwaka jana. Katika mabao hayo, 450 amefunga kwenye LaLiga yakitokana na mechi 498 alizocheza, hivyo yamemfanya kuwa mchezaji wa kwanza kwenye ligi tano kubwa za Ulaya kufikisha idadi hiyo ya mabao kwa klabu moja.

## KWA UFUPI

### SALAH AZITAJA REAL, BARCA

MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Mohamed Salah, mwenye umri wa miaka 28, amesema "majaliwa yake yapo mikononi mwa klabu" lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri amekubali kuwa anaweza kujiunga Real Madrid au Barcelona. ***(AS)***

### CITY, PSG OFA KWA MESSI

MANCHESTER City na Paris St-Germain zipo tayari kutoa ofa kwa Lionel Messi mwenye umri wa miaka 33, huku klabu hizo zikiamini kwamba mshambuliaji huyo wa Argentina ataondoka Barcelona. ***(90min)***

### JAMES HATAKI KUONDOKA UTD

WINGA wa Manchester United, Daniel James mwenye umri wa miaka 23, hayupo tayari kuondoka kwa mkopo Januari, kwani nyota huyo wa kimataifa wa Wales anataka kupigania namba pale Old Trafford. ***(Manchester Evening News)***

### PSG MAPATO HALI NGUMU

MAPATO ya Paris St-Germain kwa mwaka 2020, yanweza kuvuruga mpango wao wa kutaka kumbakiza mshambuliaji Kylian Mbappe, hata kama watauza wachezaji wengine, huku Real Madrid ikiwa tayari inasubiri kumsajili nyota huyo mwenye umri wa miaka 21 raia wa Ufaransa. ***(AS - in Spanish)***

### DEPAY NJIA NYEUPE BARCA

BARCELONA inaweza kumsajili mshambuliaji wa Lyon, Memphis Depay mwenye umri wa miaka 26, kwa bei pungufu wakati miamba hao wa Ligue 1 wakiangalia uwezekano wa kumuuza nyota huyo wa kimataifa wa Uholanzi kabla mkataba wake haujamalizika. ***(L'Equipe via Mercato)***

### LEICESTER KUMUACHIA GRAY

LEICESTER City ipo tayari kumuachia winga wake, Demarai Gray mwenye umri wa miaka 24, kundoka klabuni hapo na nafasi yake kuchukuliwa na winga wa Celtic, Ryan Christie mwenye miaka 25, au kiungo wa Reading, Michael Olise, 19. ***(90min)***

### LIVER KUMKOSA BISSOUMA

LIVERPOOL inakabiliwa na ushindani kutoka Real Madrid kwenye mbio za kumsajili kiungo wa Brighton na Mali, Yves Bissouma mwenye umri wa miaka 24, baada ya kumvutia kocha wa Madrid, Zinedine Zidane kwa kasi yake dimbani. ***(Defensa Central)***

### GIROUD AKATALIWA MILAN

AC Milan imeondoa uwezekano wa kumsajili straika wa Chelsea na Ufaransa, Olivier Giroud mwenye umri wa miaka 34, na badala yake wanataka mshambuliaji kijana kuziba pengo la majeruhi Zlatan Ibrahimovic, 39. ***(Inside Futbal)***

### DIALLO ATAKA URAIA ITALIA

WINGA wa Ivory Coast, Amad Diallo mwenye umri wa miaka 18, ameomba hati ya kusafiria ya Italia ili kufanikisha uhamisho wa pauni milioni 37.2 kujiunga na Atalanta akitokea Manchester United. ***(Sky Sports)***

### MIAMI YAMTAKA ROMERO

KLABU inayomilikiwa na David Beckham ya Inter Miami inayoshiriki Ligi Kuu Marekani, MSL, inataka kumsajili golikipa wa Manchester United, Sergio Romero mwenye umri wa miaka 33, huku raia huyo wa Argentina akitaka kuondoka pale Old Trafford. ***(Express)***

### GUENDOUZI KUBAKI BERLIN

KIUNGO wa Arsenal na Ufaransa, Matteo Guendouzi mwenye umri wa miaka 21, anaweza kuhamia kwa mkataba wa kudumu Hertha Berlin ambako yuko kwa mkopo, baada ya kocha, Bruno Labbadia kuridhika na kiwango chake. ***(Talksport)***

## HABARI MICHEZO

# KAPOMBE AAHIDI KUFA KUPONA KWA PLATINUM

**Na Saada Akida**

HUKU wakitarajia kushuka Dimba la Taifa la Zimbabwe keshokutwa, Jumatano kuwavaa wenyeji wao, FC Platinum kwenye mechi ya raundi ya kwanza ya hatua ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika, beki 'mmwaga maji' wa kulia wa Simba, Shomari Kapombe, amesema watapambana kutafuta matokeo mazuri katika mchezo huo, ili kurahisisha kazi watakaporudia.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kapombe alisema anaamini mchezo huo utakuwa na ushindani mkali kwa sababu kikosi cha FC Platinum kinaundwa na baadhi ya nyota waliowahi kucheza soka Tanzania.

Kapombe alisema uwapo wa nyota kama Thabani Kamusoko aliyewahi kuichezea Yanga, Donald Ngoma (Yanga na Azam) pamoja na Elias Maguri ambaye naye aliwahi kuichezea Ruvu Shooting, Simba, Stand United na KMC FC, kutaongeza ushindani katika mchezo huo.

"Itakuwa mechi ya ushindani ukizingatia nyota hao tumewahi kucheza nao katika ligi na timu moja, hivyo tunajuana vizuri, lakini tutapambana kutafuta matokeo chanya kuhakikisha tunafikia kile kinachotarajiwa na Wanasimba," alisema Kapombe.

Beki huyo aliwataka mashabiki kuendelea kuwasapoti katika kila mechi na wao watahakikisha wanapambana kutafuta matokeo mazuri na ikiwezekana kumaliza kazi ugenini kabla ya kurejea nyumbani katika mchezo wa marudiano.

Simba ambayo imetinga hatua hiyo baada ya kuitoa Plateau United ya Nigeria kwa bao 1-0, tayari ipo Harare, Zimbabwe tangu wiki iliyopita ikijiwinda kwa mechi hiyo kabla ya kurudiana Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam kati ya Januari 5-6, mwakani.

Endapo itaitoa FC Platinum, itatinga moja kwa moja hatua ya makundi na mechi za kwanza zitaanza kupigwa Februari mwakani.

Mchezo huo utachezwa Jumatano ya wiki ijayo, Desemba 23 ambapo utakuwa ni wa raundi ya kwanza na ule wa marudio unatarajiwa kuchezwa Dar, Januari 6.

FC Platinum imetinga hatua hiyo baada ya kuitoa Costa do Sol ya Msumbiji kwa jumla ya mabao 4-1 ikishinda 2-1 ugenini na 2-0 nyumbani.

**PAMOJA SANA...**



Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa (wa nne kulia), akiwa pamoja na Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Hassan Abbas (wa pili kushoto) na baadhi ya wafanyakazi wa Kituo cha Redio Clouds FM, ambao ni waandaaji wa Tamasha la Xtra Uni Bash lililodhaminiwa na Bia ya Guinness Smooth inayotengenezwa na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) pamoja na kampuni nyingine, muda mfupi baada ya kumalizika kwa tamasha hilo jijini Dar es Salaam jana. **MPIGAPICHA WETU**

# Mwakinyo awakataa mabondia wa ndani

**Mwandishi Wetu**

BONDIA nyota nchini, Hassan Mwakinyo, amesema Kampuni ya Jackson Group Sports imemwongezea morali ya kufanya vema zaidi katika ngumi za kulipwa nchini, huku akiweka wazi kuwa kamwe hatopigana na bondia wa ndani.

Mwakinyo alisema jana na kuweka wazi kuwa kipindi cha mlipuko wa virusi vya corona, kilimpa wakati mgumu sana kiasi cha kushuka viwango mpaka kufikia bondia wa 85 duniani.

Alisema pambano lake dhidi ya bondia Jose Carlos Paz lililoandaliwa na Kampuni ya Jackson Group Sports chini ya Ofisa Mtendaji Mkuu, Kelvin Twissa, lilimpa mwanga mpya katika ngumi za kulipwa na kukumbuka jinsi alivyopigana na bondia Sam Eggington wa Uingereza mwaka 2018 na kupanda chati mpaka kuwa miongoni mwa mabondia 15 bora duniani.

Mwakinyo alisema pambano lake na Paz lilikuwa halitabiriki na alipigana akiwa na mawazo mengi kuhusu hatima yake ya ngumi za kulipwa na hasa baada ya BoxRec kufuta baadhi ya matokeo ya mabondia nchini akiwamo.

"Baada ya kushinda dhidi ya Paz, niliwaza nini kitafuata, lakini Twissa na maofisa wa kampuni hiyo kwa kushirikiana na Rais wa WBF, Howard Goldberg, waliwasiliana na BoxRec na kufanikiwa kuweka matokeo yetu na kutatua tatizo la mabondia kuwekewa matokeo yao, hizi ni juhudi za kweli za Jackson Group Sports katika kuleta maendeleo ya kweli ya ngumi za kulipwa nchini," alisema Mwakinyo.

Alisema kwa sasa mabondia wanajua juhudi hizo zilizofanywa na Jackson Group Sports kwani awali, walikuwa kwenye giza totoro.

"Nasema nimefarijika sana kufanya kazi na Twissa na wenzake na kampuni kwa ujumla, mabondia tulikuwa njia panda, maana bila kuwa na rekodi, huwezi kupata pambano duniani," alisema.

Kuhusu kupigana na mabondia wa Tanzania, Mwakinyo alisema ni vigumu kwake kwani ni sawa na kurudi nyuma.

"Najua watu watatoa mifano ya mabondia wa Marekani na Uingereza kunipinga, lakini kiundani, sisi bado kufikia hatua hiyo na kama itakuwapo basi itatokana na ubishi wa mitaani, siyo kuendeleza mchezo wa ngumi wa ukweli," alisema.

Alisema kuna baadhi ya wadau wa ngumi wanapenda kuendekeza ubishi wa mitaani ambao hauna tija zaidi ya kutafuta 'kiki' ambazo hazina mpango katika ngumi.

## Mgosi ataka wapya wa4 Simba Queens

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi', amesema mipango yake ni kuongeza wachezaji wanne katika dirisha hili dogo ikiwamo kuwarejea nyota wao wawili ambao walizuiliwa Burundi, ili kuimarisha timu yake katika mbio za kutetea ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania.

Nyota ambao Mgosi anataka kuwaona wakirejea katika kikosi chake ni Joelle Bukuru na Asha Djafar ambao wamezuia kurejea Tanzania na Klabu ya PVP FC ya Burundi, kwa madai kuwa walisajiliwa kinyume cha taratibu.

Mgosi ameliambia gazeti hili jijini jana kuwa, kuna upungufu ameuona katika kikosi chake ikiwamo kuwakosa nyota hao ambao msimu uliopita waliitumikia timu hiyo.

Alisema mbali na nyota hao ambao wanatarajiwa kumalizana na klabu hiyo, pia wanapambana kuangalia usajili wa wachezaji wawili wengine ambao hakuweka wazi nafasi hizo.

"Kila mchezaji ana umuhimu ndani ya Simba, kutokuwapo kwa nyota hao kunaonekana pengo lao, nimekutana na uongozi kwa kuwapa mapendekezo yangu ikiwamo kumrudisha Joelle na Asha kwa kufuata taratibu ambazo wanahitaji klabu iliyowalea Burundi," alisema Mgosi.

## Ligi Daraja la Kwanza Z'bar kupigwa tena leo

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BAADA ya timu ya Jang'ombe Boys, Kilimani City na Mchangani FC kudondosha pointi katika mwendelezo wa Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja, ambayo ilianza kutimua vumbi Ijumaa iliyopita, mtifuano huo utaendelea tena leo kwa kupigwa michezo miwili.

Katika Uwanja wa Mao A timu ya Uhamiaji itaikaribisha Mchangani United, zote zikitokea Mkoa wa Mjini, mchezo utakaopigwa majira ya saa kumi alasiri, huku kwenye Dimla la Amaan, Gulioni FC ikiwa mwenyeji wa Dulla Boys ya Jambiani Mkoa wa Kusini Unguja.


Kwa upande wa mechi zilizopigwa Ijumaa, Jang'ombe Boys ilikubali kipigo cha bao 1-0 katika Uwanja wake wa nyumbani wa Mau A dhidi ya Idumu FC ya Mkoa wa Kusini Unguja wakati Mchangani FC ikiwa nyumbani nayo ilichapwa mabao 2-1 na Mwembe Makumbi City ya Mkoa wa Mjini Magharibi.

Katika Uwanja wa Kinyasini huko Mkoa wa Kaskazini Unguja, wenyeji timu ya New King walianza vema ligi hiyo inayoshirikisha timu 12, kwa kupata ushindi wa mabao 2-1dhidi ya Kilimani City yenye makazi yake mtaa wa Kilimani Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

# Michezo

Jumatatu Desemba 21, 2020

Nipashe

## PELE AMSIFU MESSI KUFIKIA REKODI YAKE

HABARI UK 22

MSITUCHUKULIE POA...



Wachezaji wa Simba, Clatous Chama (kushoto) na Joash Onyango wakiwa katika mazoezi ya timu hiyo iliyojichimbia Harare, Zimbabwe kujiandaa na mechi ya kwanza ya raundi ya Kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayopigwa nchini humo keshokutwa, Jumatano. **PICHA: SIMBA**

# PLATINUM YAONYWA SIMBA

## ●●●Nyota wakigeni waitisha wakati wakipanga ushindi wakishindo, Maguri naye asema...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI FC Platinum ikiweka wazi kuwa itapambana kufa kupona ili kuhakikisha inapata ushindi mkubwa dhidi ya Simba kwenye mechi ya kwanza ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayopigwa keshokutwa Jumatano, mabingwa hao wa Zimbabwe, wameonywa.

Simba ambayo imeitoa Plateau United ya Nigeria kwa bao 1-0 kwenye raundi ya kwanza, Jumatano itashuka katika Uwanja wa Taifa wa Zimbabwe kuvaana na wenyeji wao, FC Platinum kabla ya timu hizo kurudiana kati ya Januari 5-6, mwakani kwenye Dimba la Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Akizungumzia mchezo huo, Ofisa Habari wa FC Platinum, Chido Chizondo, amesema wamejiandaa vizuri kuhakikisha wanapata matokeo makubwa katika mchezo huo, wakiwa nyumbani kwa kuwa wanatambua ubora wa Simba inapocheza kwenye uwanja wake wa nyumbani.

"Tumejiandaa kupata matokeo mazuri, ushindi mkubwa ambao hauwezi kuwa kikwazo katika mchezo wa marudiano, tunajua Simba ni bora, lakini tutakuwa bora kwa sababu tunaanzia nyumbani," alisema Chizondo.

Kwa upande wa mshambuliaji Mtanzania Elias Maguri, aliyeifungia bao moja FC Platinum wakati ikishinda 2-1 dhidi ya Costa do Sol ya Msumbiji kwenye mechi ya raundi ya awali ugenini, alisema utakuwa mchezo mgumu kwa pande zote na atafurahi kukutana na waajiri wake wa zamani.

Maguri ambaye aliichezea Simba msimu wa 2014-2015 akitokea Ruvu Shooting kabla ya kutimkia Stand United, alisema atafurahi kuonyesha ubora wake na hahofii lolote katika mchezo huo, lakini anafahamu hautakuwa rahisi.

"Nitafurahi kama nikipewa nafasi ya kukutana na Simba niliyowahi kuichezea, na itakuwa vizuri kurudi nyumbani kwenye mechi ya marudiano na kuonyesha ubora wangu, itakuwa ni mechi ngumu," alisema mshambuliaji huyo ambaye alichangia timu yake kuitoa Costa do Sol kwa jumla ya mabao 4-1.

Lakini wakati uongozi wa klabu hiyo ya Zimbabwe pamoja na Maguri, wakieleza hayo, mshambuliaji wa zamani wa Singida United, Mzimbabwe Simbarashe Nhivi, ameionya FC Platinum kuwa makini watakapokutana na Simba Jumatano katika mchezo huo.

Nhivi maarufu kama "Simba", ambaye aliichezea Singida United msimu wa 2017-2018 kwenye Ligi Kuu Bara, ameitaka FC Platinum kuwa makini kwa kuwa Simba imeimarika kila upande huku ikiundwa na nyota wengi wa kigeni.

"Simba ni timu kubwa Tanzania kama si Yanga [Young Africans] na timu shindani sana ikiundwa na wachezaji wengi wa kigeni karibu kila idara ambao wanaweza kufunga kama wakipewa nafasi," Nhivi aliitahadharisha Platinum.

Nhivi ambaye kwa sasa anaichezea Dynamos ya Zimbabwe, aliongeza: "Kwa ujuma huwezi kuidharau timu hii. Wana ubora na wanaweza kuwa na madhara kama hawatadhibitiwa vizuri. Unapaswa kuwa mtaalamu wakati unapoivaa timu kama hii.

"Simba pia ina benchi imara la ufundi na imekuwa ikishiriki mara kwa mara michuano ya Ligi ya Mabingwa. Hivyo, kwa sasa FC Platinum inacheza na timu imara, lakini wao [FC Platinum] wana timu bora, wanaweza kuifunga timu yoyote kama wataamini wenyewe na wakiwa na kiu ya ushindi."

Platinum kwa sasa inanolewa na Kocha wa zamani wa Chippa United, Norman Mapeza, na Nhivi anaamini anaweza kufanya mambo tofauti katika mechi hizo mbili ya nyumbani na ugenini.

## KAZE KUMWONGEZEA WAWILI NTIBAZONKIZA

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imesema baada ya usajili mpya, kiungo mshambuliaji Saidi Ntibazonkiza, kuanza 'kulipa' kwa kuipa ushindi timu hiyo kwenye Ligi Kuu juzi, itaongeza wachezaji wawili zaidi kwenye kipindi hiki cha usajili wa dirisha dogo kwa ajili ya kuziba mapengo machache yaliyopo.

Akizungumza baada ya kumalizika mechi kati ya timu hiyo dhidi ya Dodoma Jiji FC, ambayo walishinda mabao 3-1, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Cedric Kaze, pamoja na mambo mengine, alisema suala la usajili lipo kwa viongozi, lakini wanapaswa kusajili wachezaji wawili ili wafunge mahesabu kwa msimu huu.

**"Mchezo haukuwa rahisi, tulifungwa bao la kwanza mapema, tukaanza kucheza kwa presha sana, badala ya kupiga pasi ili kupata njia sahihi za kushambulia tukaanza kulazimisha," alisema kocha huyo.**

Aliongeza kuwa kwa bahati nzuri walifanikiwa kupata bao la kusawazisha kipindi cha kwanza, hivyo ikawapa nafasi nzuri ya kutafuta la ushindi kipindi cha pili, vinginevyo hali ingekuwa ngumu.

Kuhusu Ntibazonkiza, alisema pamoja na kupata mchezaji ambaye anaweza kuwasaidia wenzake kwa kupenyeza pasi za mwisho, lakini atasaidia sana kwenye mipira ya faulo.

"Kwenye ligi tumekuwa tunapata faulo nyingi, lakini tulikuwa hatuzitumii vizuri, lakini sasa nadhani tumepata mtu sahihi, ndiyo maana tumemsajili ana kazi nyingi sana za kuisaidia timu," alisema Kaze.

Katika mechi hiyo, Lamine Moro, alifunga bao la kusawazisha kabla ya Ntibazonkiza kufunga la pili kwa mpira wa faulo na kisha kupiga faulo nyingine iliyounganishwa kimyani na Bakari Mwamnyeto.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002